

**NAFASI YA AINA ZA MATINI KATIKA KUSHAWISHI MBINU ZA TAFSIRI:
TATHMINI YA MWANZO, KUTOKA NA ZABURI KATIKA BIBLIA.**

**NA
OTWERA ALBERT ODIERO**

C50/81433/2015

**WASIMAMIZI
DR. ZAJA OMBOGA
BW.JOSEPHAT GITONGA**

**Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya
Shahada ya Uzamili katika
Chuo Kikuu cha Nairobi.**

2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwa maoni yangu haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi

Tarehe.....

Otwera Albert Odiero

C50/81433/2015

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi

Tarehe.....

Dkt. Zaja Omboga

Sahihi

Tarehe.....

Ndg. Josephat Gitonga

TABARUKU

Kwa mke wangu mpendwa Hellen Njeri na wanangu, Emily Mbanda, Jack Njenga na Barbara Lukale. Uvumilivu wenu, upendo wenu, hisani zenu na maombi yenu vilinitia shime katika masomo na kuniwezesha kuitimiza ndoto yangu.

Mlijinyima wakati, fedha na upendo mliohitaji kutoka kwangu ili kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Kwa haya makubwa mliyotendea, Mungu awabariki.

SHUKRANI

Kazi hii haingekamilika pasipo mkono na baraka za Mungu.,Kwa kweli amenithibitishia kwamba yeye ni mwaminifu daima. Kwa mantiki hii, natoa shukrani za dhati kwake.

Shukrani za pekee kwa wasimamizi wangu, Dkt. Zaja Omboga na Bw. Josephat Gitonga. Ushauri na mwongozo wao umekuwa wenye natija kwa utafiti huu. Mungu awabariki kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Nawashukuru sana wahadhiri wangu walioniandaa kutekeleza shughuli hii muhimu ya kiusomi: Dkt. Mwaliwa, Dkt. Zaja, Dkt. Mukhwana, Dkt. Mbuthia, Dkt. Olali, Dkt. Buregeya, Prof. Mbatia, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Habwe, Prof. Timmamy, Prof. Abdulaziz na Bw. Mungania. Sina budi pia kuwashukuru wahadhiri wengine ambao ijapokuwa hawakunifunza walitoa mchango wao kwa ushauri ulionifaa kwa njia yoyote ile.

Aidha nina shukrani za pekee kwa wanafunzi wenzangu tulioshirikiana nao bega kwa bega katika safari hii: Ngulamu Mwaviro, Joshua Anusu, Samuel Ngunyi, Zipporah Kitiku Edwin Muna, Lillian Chacha na Purity Kolongei, Katu sitawasahau katika mustakabali wangu. Bila shaka nitalikosa darasa letu.Mungu awabariki na kuwafanikisha katika mipango yenu ya siku za usoni.

Sitawasahau mchango wa jamaa zangu wengine. Babangu mpendwa Jackson Otwera; kaka zangu Massanga, Obare, Omurumba, Owende na Acheru; dada zangu Atsali na Isabella. Asanteni sana kwa malezi yenu na maombi yenu. Msaada wenu kwangu hauna kifani.

YALIYOMO

Ungamo	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Yaliyomo	v
Orodha ya Vifupisho	ix
Ikisiri	x
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti	4
1.2 Malengo ya Utafiti	4
1.3 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.4 Upeo na Mipaka	5
1.5 Msingi wa Kinadharia	6
1.5.1 Nadharia ya Tafsiri Kielimumtindo.....	6
1.6 Nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano.....	7
1.6.1 Ukopaji.....	8
1.6.2 Ulinganifu wa Kitamaduni.....	8
1.6.3 Ulinganifu wa Kiuamilifu	8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.....	9
1.8 Njia za Utafiti.....	11
SURA YA PILI: HISTORIA YA BIBLIA	12
2.0 Utangulizi	12
2.1 Fasili ya Matini za Kidini	12
2.2 Chimbuka la Dini ya Kikristo	13
2.3 Ulimwengu wa Biblia.....	14
2.3.1 Ndoa na Familia za Wayahudi	15
2.3.2 Elimu ya Wayahudi	16
2.3.3 Vyakula na Vinywaji	16
2.3.4 Amali za Wapalestina	17
2.3.5 Maisha Vijijini na Mijini.....	18

2.3.6 Usafiri katika Palestina	19
2.3.7 Sherehe na Siku Takatifu	20
2.3.8 Hekalu	20
2.3.9 Muziki na Sanaa	21
2.4 Uandishi wa Agano la Kale	22
2.4.1 Miswada ya Agano la Kale	22
2.4.2 Tafsiri za Kwanza za Biblia	23
2.5 Uandishi wa Agano Jipya	23
2.5.1 Tafsiri za Biblia Baada ya Mitume.....	24
2.5.2 Tafsiri za Kiingereza	25
2.6 Biblia na Mageuzi	25
2.7 Tafsiri za Kisasa za Biblia	26
2.8 Tofauti za Kihistoria za Wafasiriwa Biblia	26
2.9 Historia ya Biblia ya Kiswahili.....	27
2.10 Biblia ya Kikristo na Apokrifa.....	31
2.11 Biblia na Ufeministi	31
2.12 Biblia na Usasaleo.....	32
2.13 Muhtasari	32
SURA YA TATU:MATINI ZA BIBLIA	33
3.0 Utangulizi	33
3.1 Matini Chanzi za Agano la Kale	33
3.2 Matini Chanzi za Agano Jipya.....	33
3.3 Mbinu za Uhakiki wa Matini za Kibiblia	34
3.3.1 Uhakiki wa Kihistoria	34
3.3.2 Uhakiki wa Kimatini.....	34
3.3.3 Uhakiki wa Chanzo.....	35
3.3.3.1 Chanzo cha Yahwist.....	36
3.3.3.2 Chanzo cha Elohist	36
3.3.3.3 Chanzo cha Ki-Priest	37
3.3.3.4 Chanzo Ki-Deuteronomy	37
3.3.3.5 Chanzo cha Marko na Q.....	38

3.3.4 Uhakiki wa Umbo.....	39
3.3.5 Uhakiki wa Ki- Historia Mapokeo	39
3.3.6 Uhakiki Hariri.....	40
3.4 Aina za Matini za Tafsiri	41
3.4.1 Matini ya Kimjadala	42
3.4.2 Matini Fasili	42
3.4.3 Matini Elekezi	42
3.4.3.1 Usahili	43
3.4.3.2 Utopiki.....	43
3.4.3.3 Ukumbukwaji	43
3.4.3.4 Uvutiaji.....	43
3.4.3.5 Utekenyaji Hisia	43
3.4.3.6 Unyumbuaji wa Lugha.....	44
3.4.3.7 Kuaminika	44
3.4.4 Masimulizi.....	44
3.4.4.1 Masimulizi ya Kisayansi	44
3.4.4.2 Masimulizi ya Umma.....	45
3.4.4.3 Masimulizi ya Kiontolojia.....	45
3.4.4.4 Masimulizi Dhanifu	46
3.4.4.5 Masimulizi ya Kimataifa.....	46
3.4.5 Mashairi.....	47
3.4.6 Dayalojia	49
3.4.7 Matini Fafanuzi.....	49
3.5 Muhtasari	49
SURA YA NNE:NAFASI YA AINA ZA MATINI KATIKA KUSHAWISHI MBINU ZA	
TAFSIRI	51
4.0 Utangulizi	51
4.1 Uchanganuzi waTafsiri ya Zaburi 23	51
4.2 Uchanganuzi wa Tafsiri ya Mwanzo II	54
4.3 Uchanganuzi wa Tafsiri ya Kutoka 20	56
4.4 Muhtasari	60

SURA YA TANO:MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	61
5.0 Utangulizi	61
5.1 Muhtasari	61
5.2 Matokeo	62
5.3 Mapendekezo	63
MAREJELEO	65

ORODHA YA VIFUPISHO

HL	-	Hadhira Lengwa
MC	-	Matini Chanzi
ML	-	Matini Lengwa
LC	-	Lugha Chanzi
LL	-	Lugha Lengwa
KJV	-	King James Version
SUV	-	Swahili Union Version
BHN	-	Biblia Habari Njema
AK	-	Agano la Kale
AJ	-	Agano Jipya
LXX	-	Agano la Kale la Kiyunani
SSBE	-	Sacred Scriptures Bethel Edition

IKISIRI

Suala la ulinganifu katika tafsiri si la kiwango cha maneno na sentensi pekee yake. Uelewa wa vipengele vingine vya ulinganifu kama vile aina za matini na rejesta una natija kwa mfasiri kwa kuwa humwezesha kubaini mbinu mwafaka ya kutafsiri matini ya aina fulani anayoishughulikia. Utafiti huu umeshughulikia nafasi ya aina za matini na nduni zake katika kushawishi mbinu za tafsiri kwa kutathmini vitabu vya Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23. Dhana ya aina za matini imefafanuliwa kwa kina. Tumeainisha aina kadha za matini na kuonyesha jinsi ambavyo nduni zake zinavyoshawishi mbinu za tafsiri. Tumeonyesha umuhimu wa upekee na umbo la kila matini na uamilifu wake wa kimawasiliano katika uhawilishaji wa ujumbe wa matini chanzi.

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Kila mfasiri ana jukumu la kutambua aina ya matini anayoifasiri ili kufanikishia upatikanaji wa tafsiri inayoakisi maana iliyokitwa katika matini chanzi (tangu sasa MC). Hivyo uanishaji wa matini za tafsiri katika makundi mbali mbali ni shughuli ya lazima katika taaluma ya tafsiri kwa kuwa ndiyo inayoukilia mbinu mwafaka ya tafsiri. Matini za tafsiri zinaweza kuanishwa katika makundi matatu makuu kwa kuzingatia dhima kuu tatu za lugha- matini elezi, matini arifu na matini amili. Matini elezi huegemea zaidi kwa mwandishi na kumpa hadhi ya “mtakatifu.” Mwandishi hutumia lugha kuelezea hisia zake bila kujali jinsi maelezo hayo yatakavyopokelewa na hadhira, yaani wasomaji. Mifano ya matini elezi ni kazi za fasihi zilizobuniwa kwa makini, kama vile ushairi, hadithi fupi, tamthilia na riwaya; kauli za kimamlaka au kimadaraka, kama vile Maandiko Matakatifu, hotuba na nyaraka za kisiasa (mathalan za marais, magavana, n.k), nyaraka za kisheria, kazi za kisayansi, kifalsa na kitaaluma zilizoandikwa na wataalamu walioboea; wasifu nafsi, insha na mawasiliano ya kibinafsi baina ya watu. Aghalabu matini elezi zinahusu imani za waandishi na zina madai ya kiusomi.

Matini arifu zinahusu mada yoyote ile ya maarifa, kwa mfano sayansi, teknolojia, biashara, uchumi n.k. Umbo la matini arifu huwa ni sanifu, mathalan, vitabu, ripoti za kiufundi, makala katika magazeti, majarida ya kitaaluma, tasnifu, madondoo ya ajenda za mikutano au kumbukumbu za mikutano na kadhalika. Matini amili zimeegemea zaidi upande wa hadhira, yaani wasomaji. Matini hizi hulenga kuibua hisia za msomaji na kumfanya afikiri au atende kwa namna ambayo imekusudiwa na matini mahususi. Mifano ya matini amili ni pamoja na matangazo, maelekezo, propaganda, maombi, mialiko na fasihi pendwa. Hata hivyo ni muhimu kutaja kwamba kuna matini chache sana ambazo ni elezi, arifu au amili tu. Matini zilizo nyingi zina mchanganyiko wa sifa zote, huku mojawapo ikiwa ndiyo inayojitokeza zaidi ya nyingine. Kwa mfano, matini arifu zilizo nyingi huwa na hali ya uamili ndani yake; matini haiwezi kuwa arifu tupu. Hali kadhalika matini huweza kuanishwa kufuatana na mada. Kwa kutumia kigezo hiki tunaweza kuzigawa matini za tafsiri katika makundi matatu; matini za kifasihi; matini za kiasasi kama vile, dini, siasa, biashara, fedha, serikali, n.k; matini za kisayansi, zinazohusu nyanja zote za sayansi na teknolojia.

Kama tulivyotaja hapo awali uanishaji wa matini katika makundi mbalimbali ni muhimu kwani aina mahususi ya matini ndiyo inayayoukilia mbinu mwafaka ya tafsiri. Kwa mfano, matini amili huwa na mwelekeo wa kutafsirika zaidi kwa kutumia tafsiri ya kimawasiliano (tafsiri huru) kwa kuwa mbinu hii hufanikisha upatikanaji wa tafsiri nyepesi inayoingiliana na utamaduni wa hadhira lengwa (tangu sasa HL). Aidha pale zoezi la tafsiri linapofanyika kibiashara, gharama za tafsiri hupangwa kulingana na aina ya matini inayofasiriwa. Mathalan, matini za kiufundi, hulipiwa gharama kubwa zaidi kuliko matini zisizo za kiufundi. (Mwansoko, Mekacha, Masoko & Mtesigwa 2015:13). Kwa kuzingatia kigezo cha asasi, Biblia huweza kuanishwa kama matini ya kidini. Matini ya kidini ni matini ambayo kwa mujibu wa mapokeo fulani ya kidini huchukuliwa kuwa msingi wa maisha fulani ya kidini au seti ya itikadi zake. Nduni zinazobainisha matini ya kidini ni kama vile matumizi ya lugha ya kimamlaka, uwezo wa kujifasiri uliokitwa katika matini yenyewe, urejelezi ulio wazi na urejelezi fiche, mwingiliano matini, uwezo wa matini kudhibiti tafsiri yake (metatextuality) na ufasiri wa kimifano (typological interpretations). Mathalan, kwa mujibu wa mapokeo ya dini ya Kikristo, Biblia ni matini ya kimamlaka ambapo uhalali wa mamlaka yake umekita ndani mwake, na chimbuko lake huchukuliwa kuwa ni Mungu. (<https://en.m.wikipedia.org.>wi>).

Aidha Biblia ni orodha (canon) ya matini sitini na sita za kidini ambamo sifa ya mwingiliano matini inabainika kwa kuwa matini zinachangizana katika kufanikisha uelewa wa msomaji. Hivyo Agano la Kale huwezesha uelewa wa Agano Jipya na Agano Jipya hufanikisha uelewa wa Agano la Kale. Orodha hii ya matini katika Maagano haya mawili huchukuliwa kuwa hazina ya kweli na maadili ambayo ni kamilifu na isiyobadilika (ndiyo sababu Wakristo wanaitambua kama “Kanuni ya Imani”). Maana ya matini yoyote kwa mujibu wa Aichele (2001:9) hukitwa katika matini yenyewe. Hivyo Biblia imesheheni maana zinazoiwezesha kusema na kila wakati na watu wote kwa kuwa ni aina ya matini “takatifu” isiyopitwa na wakati. Hali kadhalika mfano wa urejelezi ulio wazi katika Biblia ni kama vile katika Mariko 14:48-49 ambayo inanukuu maneno ya Agano la Kale na istilahi zinazohusiana nalo (mathalan “sheria na maanabii”) huku urejelezi fiche ukionekana katika mfano wa matumizi ya “Mwana wa Adamu” (Mathayo 24:37) kutokana na kitabu cha Danieli 3:25. Tafsiri za kimifano zinaonyesha uhusiano baina ya aina za matini na mbinu zinazotumika kuzifasiri.

Mathalan pana uhusiano kati ya kisa cha mnara wa Babeli na kile cha Siku ya Pentekote ambavyo vinafanana kimasimulizi, hivyo huweza kutafsiriwa kwa njia zinazoshabihiana. Kwa jumla, Biblia ni orodha ya matini yenye ukwasi wa mwingiliano matini na uwezo wa kudhibiti tafsiri yakeunaowezesha kupunguzwa kwa changamoto za uelewa ama kwa mfasiri au msomaji. Hizi ndizo sifa pekee zinazoitambulisha Biblia miongoni mwa matini nyingine za kidini.

Biblia ina aina kadha za matini zinazokilia mbinu zinazotumika kuzitafsiri: mathalan masimulizi, maelezo, linganifu (comparative), mashairi, elekezi (prescriptive) na dayalojia. Masimulizi huwa na ploti, wahusika, mazingira na maudhui. Vitabu vingi katika Agano Kale, mathalan Wafalme wa Kwanza na Wafalme wa Pili ni matini za kimasimulizi. Matini ya kimaalezo hutoa maelezo ya kimuktadha kuhusu mtu, kitu, mahali au shughuli fulani. Mfano mwafaka wa matini ya kimaalezo ni Mambo ya Walawi 16 ambamo Mungu anatoa maelezo kuhusu Sherehe ya Siku ya Upatanisho. Aidha Wimbo Ulio Bora ni matini linganifu kwa kuwa uhusiano wa mume na mke umelinganishwa na uhusiano wa Mungu na Kanisa. Mifano ya matini ya kishairi ni kama vile Zaburi na Ayubu na mifano ya matini elekezi ni kama vile Kutoka sura ya 20 (yenye amri kumi za Mungu) na Mathayo sura ya 5 ambamo Yesu anawaamrisha Wakristo jinsi ya kuishi duniani. Aidha kitabu cha Ayubu sura ya 4 hadi 14 ni dayalojia kati ya Ayubu na rafikize (Elifazi, Bildadi, Sofari na Elihu) kuhusu kiini cha masaibu ya Ayubu.

Zipo tafiti kadha ambazo zimewahi kufanywa kuhusu suala la kutafsiri matini ya kidini kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Mathalan, utafiti wa Ondara (2010) uliokitwa katika ufaafu wa maana katika tafsiri ya nyimbo dini za Kikristo kutoka Kingereza hadi Kiswahili ulibaini kuwa baadhi ya nyimbo dini hupoteza, huongeza au kubadili baadhi ya maana katika ML kutokana na mapungufu kama vile kuingizwa kwa vipengele visivyokuwa katika MC, matumizi ya msamiati usio linganifu, kuzingatia muwala kuliko maana na makosa ya kisarufi. Licha ya kupendekeza wafasiri walinganishe nyimbo dini na tanzu nyingine za fasihi (mathalan mashairi) na historia zao ili kupata uelewa wa vipengele vyake muhimu na utamaduni wa LC, utafiti wa Ondara haukushughulikia suala la mtindo wa matini kama kigezo kinachokulia mbinu ya tafsiri inayostahili kutumika.

Hali kadhalika mwanya huu umedhihirika katika utafiti wa Otwere (2011) uliotathmini usonde katika kitabu cha Mafundisho ya Biblia kwa Watu Wazima katika Seventh Day Adventist Church kwa msingi wa nadharia ya Umaanisho na kupendekeza wafasiri wa matini ya kidini watafiti kuhusu maneno ya usonde (usonde jamii, usonde matini, usonde diskosi na usonde wakati) na sifa zao ili kufanikisha tafsiri zaidi. Tafiti hizi chache zimeonesha kuwa aina za matini ya kidini na jinsi zinavyoshawishi mbinu za tafsiri hazijapewa kipaumbele katika usomi wa tafsiri. Tumehoji kwamba nadharia ya Umaanisho haitatupa msingi mwafaka katika kutathmini mtindo kama kigezo kinachoukilia mbinu za kutafsiri matini ya kidini hususan Biblia hivyo utafiti wetu umekitwa katika nadharia mbili: nadharia ya Tafsiri Kielimumitindo (Stylistic Translation) na nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano (Communicative Translation). Ili kupata data ya msingi yenye msambao mwafaka tumetathmini kitabu cha Mwanzo sura ya 11 kama matini teule ya kimasimulizi, kitabu cha Kutoka sura ya 20 kama matini teule elekezi (prescriptive text) na kitabu cha Zaburi sura ya 23 kama matini teule ya kishairi.

1.1 Tatizo la Utafiti

Kila mradi wa kutafsiri ni sharti ufanywe kwa kuzingatia aina na mifumo ya matini. Hii ina maana kwamba mfasiri anashurutika kuangazia mambo yanayohusiana na lugha ya MC kama vile masimulizi, uelekezi, uelezaji, ulinganishaji, ufafanuzi, na dayalojia ; aina za matini (mathalan za kidini, za kisheria na za kifasihi), sifa na visifa vinavyozitambulisha; na aina ya utanzu wa matini inayofasiriwa kama vile nathari, dayalojia na ushairi. Tafiti nyingi za awali kuhusu ufasiri wa matini ya kidini hususan Biblia zimeonekana kutoshughulikia suala la aina za matini ya kidini katika kushawishi mbinu zinazotumika kuzitafsiri. Utafiti wetu ulilenga kuziba mwanya huu kwa kutathmini nafasi ya aina za matini katika kuikilia mbinu zinazotumika kufasiri kwa mintoarafu ya vitabu vya Mwanzo Sura ya II, kutoka sura ya 20 na Zaburi sura ya 23.

1.2 Malengo ya Utafiti

- (i) Kuchunguza aina na sifa za matini ya kidini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23.
- (ii) Kuchunguza nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za kutafsiri matini za kidini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23.

(iii) Kutambua mbinu za kutafsiri matini ya kidini zinazoshawishiwa na aina za matini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23.

1.3 Maswali ya Utafiti

- (i) Je ni aina gani za matini ya kidini zinazopatikana katika Mwanzo 11, Kutoka 20 na Zaburi 23?
- (ii) Ni vipi aina hizi za matini zinazawishi mbinu za kuzitafsiri?
- (iii) Ni mbinu zipi za tafsiri zilizoshawishiwa na mitindo ya Mwanzo 11, Kutoka 20 na Zaburi 23?

1.3 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti wetu umekitwa katika msingi kuwa kila MC sharti ichunguzwe kama matini ngeni iliyo na upekee wa aina yake ili kumwezesha mfasiri kutambua aina ya matini anayoifasiri hivyo kutumikiza mbinu mwafaka ya kutafsiri inayoakisi upekee wake. Kama tulivyotaja katika utangulizi wetu Biblia ni mkusanyiko wa aina mbali mbali za matini ya kidini hivyo inaweza kutegemewa katika kuzalisha data yenye mashiko kwa msingi ya nadharia za Tafsiri Kielimumtindo na Tafsiri Kimawasiliano. Tumehoji kuwa vitabu vya Mwanzo, Kutoka na Zaburi ni matini za kidini, kila kimojawapo kikiwa na upekee wake ambao huweza kuikilia mbinu ya kuifasiri. Uelewa wa wafasiri kuhusu aina za matini ya kidini na ushawishi wake kwa uteuzi wa mbinu za kutafsiri ni swala ambalo kutokana na mapitio yetu ama halijapewa kipaumbele ama halijashughulikiwa kwa upana.

Aidha tumehoji kuwa utafiti wetu utawezesha taaluma ya tafsiri kupata ilhamu kwa kuwa utambuzi wa aina ya matini ya kidini inayofasiriwa utamwezesha mfasiri kuepuka kuingiza chukulizi mpya kwenye MC.

1.4 Upeo na Mipaka

Kiini cha utafiti wetu ni kaida za matini za kidini zinazopatikana katika Biblia kama kigezo cha kushawishi mbinu za kuzitafsiri. Ijapokuwa masuala kama vile rejesta, utamaduni na historia ya LC na ulinganifu wa maana kati ya MC na ML ni masuala muhimu katika ufasiri wa matini ya kidini hususan Biblia na yana mwingiliano fulani na utafiti wetu, tuliyapembeza na kukita katika mitindo ya matini ya kidini na aina zake ili kupata mkakati wenye dira utakaolekeza utafiti

wetu. Mitindo ya matini ya kidini katika Biblia ni kama vile masimulizi, dayalojia na mashairi na inahusika pakubwa katika kuelekeza maana na kufaulisha uhamishaji wa ubora na MC hadi ML. Tuliteua Biblia kama data yetu ya msingi kwa kuwa kwa mujibu wa tafakuri yetu utafiti wetu ungefaidi kutokana na ukwasi wake wa aina za matini na kaida zake hususan tafsiri za KJV na SUV.

1.5 Msingi wa Kinadharia

Katika utangulizi wetu timetaja kuwa utafiti wetu ungeongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Tafsiri Kielimumtindo na Nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano. Nadharia hizi mbili zilikuwa na natija kwa utafiti wetu kwa kuwa zimetuwezesha kutathmini vipengele viwili muhimu vya tafsiri; mtindo na maana. Mfasiri anashurutika kuzingatia mwingiliano wa karibu kati ya mtindo na maana ili kufanikisha upatikanaji wa tafsiri inayoafiki ujumbe wa MC kimtindo na kimaana. Kubaini mtindo wa MC kwa mujibu wa Mwansoko n.w (2015:16) ni suala muhimu kwani nadharia ya tafsiri inasisitiza mitindo ya matini chanzi ilingane na ile ya ML. Aidha dhima ya tafsiri katika kunafinikisha mawasiliano imetupa sababu nzuri ya kuhoji kuwa utafiti wetu imefaidi kutokana na nadharia ya mawasiliano.

1.5.1 Nadharia ya Tafsiri Kielimumtindo

Nadharia ya Elimumtindo imekitwa katika dhana kuwa kila matini ina upekee wa vipengele mahususi na miundo au aina za vipengele na miundo ipatikanayo katika lugha. Taaluma hii inahusu uanishaji wa mitindo ya lugha na miktadha ya matumizi yake katika MC. Tafsiri ya kielimumtindo itamwezesha mfasiri kubaini mtindo wa MC yake ambao hauna budi uhamishwe kwenye ML. Nadharia hii inasisitiza kuwa mitindo ya MC na ML ilingane (Malmjaer 2004:550). Kwa mantiki hii dhamana ya mfasiri wa matini ya kidini sharti iwe kwenye LC yaani ya mwandishi. Hii ina maana kwamba matini ya kishairi kama vile Zaburi haina budi kutafsiriwa kwa kutumia tafsiri ya kisemantiki kwa kuwa tafsiri ya kisemantiki huwekea mkazo kwenye maana ya MC kama ilivyokusudiwa na mwandishi. Mfasiri hulenga kuhifadhi mtindo na maana iliyokusudiwa na mwandishi kwa kufuata miundo ya kisemantiki na kisintaksi ya LL. Tuchunguze mfano ufuatao kutoka kitabu cha Zaburi sura ya 1 mstari wa 1:

Matini ya Kiingereza

*Blessed is the man
that walketh not in the counsel of
the ungodly,
nor standeth in the way of
sinners,
nor sitteth in the seat of the
scornful.(KJV)*

–

Tafsiri ya Kiswahili:

Heri mtu Yule asiyekwenda
Katika shauri la wasio haki;
Wala hakusimama katika njia ya wakoaji;
Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.
(SUV)

Kutokana na mfano huu ni bayana kuwa mfasiri amehifadhi mtindo wa MC bila masahihisho ya kinachofikiriwa kimepotoshwa katika MC au uboreshaji wa aina yoyote wa MC katika tafsiri hii kwa kuwa hivi havina nafasi katika tafsiri ya kisemantiki. Kwa mujibu wa Boase-Beier (2012) nadharia hii imekitwa katika maana ya namna (*the how meaning*) wala si maana ya nini (*the what meaning*) ya M.C. Baadhi ya nduni za maana ya namna ni kama vile utata, kauli tendwa, kauli tendewa na urefu wa sentensi. Mtindo wa matini huakisi umbuji wake wa kisanaa ambao una uwezo wa kuathiri msomaji kwa kuzitekenya hisia zake.

1.6 Nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano

Nadharia ya tafsiri kimawasiliano inasisitiza kumlenga msomaji wa ML ambaye hatarajii ugumu wowote katika matini atakayoisoma, bali hutarajia tafsiri nyepesi ya dhana za kigeni katika utamaduni na lugha yake kila inapolazimu na kwa kadiri inavyowezekana. Tafsiri ya kimawasiliano hulenga kutoa athari ile ile au inayokaribiana kwa hadhira ya tafsiri kama ilivyokuwa kwa hadhira ya MC.

Dhima ya nadharia hii kwa mujibu wa Mwansoko n.w (2015:28) imekitwa katika matini zinazotoa ujumbe wa jumla, usiofungamana na utamaduni wa LC na pale ambapo maudhui ni muhimu sawa na muktadha, mathalan katika matini muhimu za kidini, kisiasa, kifalsafa na kisayansi. Hii ni kwa sababu mahitajio na matarajio ya hadhira ya LL kwa mada hizo hayatofautiani na yale ya hadhira ya LC. Mfasiri yuko huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa. Hivyo licha ya tafsiri ya kimawasiliano kufuata sarufi ya lugha ya pili (LL), ni lazima ifuate pia

mwelekeo wake wa kijamii, kihistoria, kitamaduni na kimazingira; Tafsiri ya kimawasiliano hutumika sana kufasiri mambo au mawazo ya kigeni katika lugha na mazingira mapya, mawazo ambayo huelezwa katika misingi ya lugha, utamaduni na mazingira yanayoeleweka kwa wasomaji wa LL. Matumizi ya mawazo ya kigeni kwa Kiswahili katika Biblia (mathalan, misemo inayohusiana na baadhi ya vyakula) yanahalalisha matumizi ya nadharia hii katika utafiti wetu (Taz. Malangwa 2014: 104). Nadharia hii ina mihili mitatu muhimu:

1.6.1 Ukopaji

Ukopaji ni kitendo cha mfasiri kuchukua maneno au utaratibu wa kiusemaji wa lugha moja kisha kuutumia na hatimaye ukawa sehemu ya lugha hiyo. Mfano wa ukopaji wa maneno ni ule wa neno *mana* (Kumbukumbu la Torati 8:15, Yohana 6:31 na Ufunuo 2:17) ambapo neno hili limeingizwa katika Kiswahili kutoka Kiebrania kwa kuwa misemo ya utamaduni wa Kiswahili wa vyakula haina neno hili.

Aidha mfano wa ukopaji wa kiusemaji ni ule wa matumizi ya usemi kama “tohara...ya...moyo” katika kitabu cha Warumi 2:29 (kwa maana ya kuongoka) ambapo maneno yaliyopigiwa msitari yametokana na maneno ya Kiingereza “circumcision of the heart.” (Massamba 2009:100).

1.6.2 Ulinganifu wa Kitamaduni

Hapa ni pale ambapo mfasiri anashurutika kutafsiri neno litokanalo na utamaduni wa LC kwa neno la utamaduni wa LL kwa kadiri inavyowezekana ili kutoa athari ile ile au inayokaribiana kwa hadhira ya tafsiri kama ilivyokuwa na hadhira ya MC. Mathalan neno “*believe*” imetafsiriwa kama *amini* kwa maana ya kukubali kwamba jambo ni la kweli (Mathalan, Mathayo 9:28 na Waebrania 11:6). Ulinganifu wa kitamaduni ni muhimu kwa kuwa hutoa athari ya moja kwa moja kwa HL.

1.6.3 Ulinganifu wa Kiuamilifu

Ulinganifu wa kiuamilifu ni utaratibu unaotumika kwa maneno ya kitamaduni ambapo mfasiri anahitajika kutumia neno au istilahi isiyofungamana na utamaduni wowote hivyo kuifanya istilahi hiyo kuingiliana na tamaduni zote mbili au kuwa neno jumla. Kiini cha kanuni hii kwa mujibu wa Kirk (2005:90) ni mtazamo ya maana kwa maana ambapo mfasiri anawasilisha

ujumbe uliowasilishwa kwa hadhira ya MC. Kanuni hii inahusu matimuzi ya utaratibu wa uchanganuzi vijenzi na huwezesha ufaafu wa maana za maneno hususan ya kitamaduni. (Muruga, 2012). Kwa mfano neno “*tenderhearted*” (Waefeso 4:32) limetafsiriwa kama *wafadhili* hivyo maana ya MC ikahamishwa hadi ML.

Katika kuhitimisha mjadala huu tumekubaliana na mawazo ya Delabastita (1993:42-44) kuwa nadharia hii ina hoja tatu muhimu: kuyatendea haki malengo ya mwandishi wa MC, kuhifadhi kwa kadiri iwezekanavyo thamani ya ukweli wa mawazo ya MC na kuwianisha hadhira ya matini chanzi na ile ya matini lengwa.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii

Sehemu hii imeangazia kazi za awali zinazohusu tafsiri za matini ya kidini hususan zinazoegemea mitindo ya masimulizi, uelekezi na mashairi. Hali kadhalika tumejadili michango ya wasomi wengine kuhusu nadharia za Tafsiri Kielimumtindo na Tafsiri Kimawasiliano kwa kuwa kiini cha utafiti wetu ni kupata majibu kuhusu nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri. Ingawa tafiti za Ondara (2010, Ufaafu wa Maana katika Nyimbo Dini) na Otwere (2011, Usonde katika Tafsiri: Tathmini ya Mafundisho ya Biblia katika Shule ya Sabato kwa Watu Wazima) zilitoa mchango wa kiusoni kwa kutathmini masuala yanayohusu ulinganifu wa maana katika tafsiri za matini ya kidini hazikushughulikia dhima ya mtindo katika kushawishi mbinu za kutafsiri. Aidha Mwansoko n.w (2015:48) anadai kwamba mojawapo wa sababu zinazochangia mapungufu katika tafsiri za kutoka lugha nyingine (hususan Kiingereza hadi Kiswahili) ni kuwa bado Kiswahili hakijawa na uwezo mkubwa wa kutofautisha mitindo mbalimbali iliyokwishaajibainisha katika lugha zilizoendelea. Ametetea kauli hii kwa kutoa mifano ifuatayo:

Matini ya Kiingereza

Thou shalt not steal

(Mtindo wa Kidini)

Do not steal (kawaida)

Lend me your ears

Tafsiri ya Kiswahili

Usiibe

Usiibe

(Mtindo wa Kishairi)

Naomba mnisikilize

May I have your attention (kawaida)

Naomba mnisikilize

Tafsiri zilizotolewa hapo juu zinaonyesha kuwa mfasiri ametumia mbinu ya tafsiri huru kutoa maana japo ameuza mtindo. Hali kadhalika tafsiri iliyopo hapa chini inaonyesha matumizi ya mbinu ya neno kwa neno ili kuhifadhi mtindo wa MC:

“While we are trying to help him he continues to abuse us.

(mtindo wa maandishi)

(a)Pale ambapo tunajaribu kumsaidia yeye anaendelea kutokana

(b)Ingawa tuna.....

(c)Wakati tuna.....

(d)Wakati ambapo tuna.....

Tafsiri hizi, japo zinazingatia mtindo wa MC, hata hivyo hazitoshelezi kutoa dhana ya neno *while*, yaani tofauti za matendo na mshangao sawa. Dhana hiyo inaweza kutolewa tu kwa kutumia neno “huku” (na ikilazimu pia kiunganishi “na”) ambalo matumizi yake aghalabu hujitokeza kwenye mtindo wa mazungumzo:Huku tunajaribu kumsaidia (na) yeye anaendelea kututukana. Hata hivyo madai kwamba Kiswahili hakina uwezo mkubwa wa kutofautisha mitindo mbalimbali hayana mashiko kwa kuwa zipo mbinu kadha ambazo mfasiri anaweza kutumia kuhifadhi mtindo wa MC na maana yake. Mathalan, kuepuka kuunda istilahi ambazo, tayari, zina istilahi zenye kuziwakilisha, kutumia vya kutosha hazina ya maneno ya Kiswahili iliyopo kwawazungumzaji wa Kiswahili badala ya kutohoa (tazama mfano hapo juu) na kuunda istilahi zinazoweza kueleweka kwa urahisi.

Tathmini ya Boase-Beier (2012) kuhusu nafasi ya elimumitindo katika kufanikisha ufaafu wa maana katika tafsiri imetoa mchango mkubwa kwa utafiti wetu. Anahoji kuwa uwezo wa matini kuathiri hadhira yake unatokana na lile umbo lake maalum. Hii ni kwa sababu mtindo wa matini hutoa maana maalum isiyopatikana katika elementi leksika na sintaksi ya LC na LL. Umuhimu wa matini tafsiri haumo katika umatini wake tu bali na katika upekee wa kategoria yake na hivyo uamilifu wake huchangiwa kwa kiasi fulani na mtindo wake unaoshahibiana na MC. Ni kwa mantiki hii ambapo tafsiri yoyote yenye lengo ama la kuhifadhi mtindo wa MC au kubadili

mtindo wake itahitaji kuwiana na mtindo wa MC. Mathalan, mfasiri wa matini ya kishairi atahitajika kwa kadiri iwezekanavyo kuhifadhi elementi za ushairi kama vile utata, mpangilio na sauti wenye mapigo ya kimuziki na wizani, maelezo mafupi, na yenye kunata, matumizi bora ya picha, ishara na tamathali za semi na ukiushi wa kisintaksia. Aidha mtindo wa matini kwa mujibu wa Boase-Beier huakisi msingi wa kitamaduni wa MC na hujenga taswira ya wasomaji wa MC na ML. Kutokana na tathmini ya mapitio yetu tunahoji kuwa kuuza, kuongeza au kupunguza upekee wa mtindo wa matini ya kidini huathiri thamani ya ML kwa hadhira yake hivyo mfasiri anashurutika kuhifadhi mtindo wa MC kwa kadiri iwezekanavyo kwa kubaini ni mbinu ipi ya tafsiri itakayofanikisha uelewa wake.

1.8 Njia za Utafiti

Data za msingi katika utafiti wetu zimetokana na matini tatu katika Biblia: Kitabu cha Mwanzo sura ya II kama kiwakilishi cha matini ya kimasimulizi, kitabu cha Kutoka sura ya 20 kama kiwakilishi cha matini elekezi na kitabu cha Zaburi sura ya 23 kama kiwakilishi cha matini ya kishairi. Tunahoji kuwa matini hizi za AK ni maarufu miongoni mwa Wakristo.

Tumekita katika nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za kutafsiri kwa kutathmini matini hizi teule katika tafsiri ya *King James Version* ya Kiingereza na tafsiri ya *Swahili Union Version* ya Kiswahili ambayo ndiyo mshabaha wake. Tulichagua tafsiri ya KJV kwa kuwa yamkini ndiyo matini ya Kiingereza yenye ukwasi mkubwa zaidi wa mitindo. (Taz. Goswell 2011 na Alter 2010). Matokeo ya utafiti wetu yamewasilishwa kwa njia ya maelezo pamoja na mapendekezo.

Tumetumia maktaba kukusanya data za upili: vitabu, makala, majarida na tahakiki, hususan zinazojadili tafsiri za matini za kidini, mitindo yake na ushawishi wa mitindo hii kwa mbinu za tafsiri. Aidha tumekusanya data zinazojadili nadharia ya tafsiri, fasili za matini ya kidini na aina zake na historia ya tafsiri ya Biblia kisha kuzitumikiza katika kutathmini data za msingi katika vitabu vya Mwanzo, Kutoka na Zaburi.

SURA YA PILI HISTORIA YA BIBLIA

2.0 Utangulizi

Historia ya Biblia na waandishi wake vimetupa ufahamu kuhusu mtindo wa MC na *maana ya namna* ambayo mwandishi alitaka kupitisha kwa hadhira yake, hivyo kutambua ikiwa imejitokeza katika ML, imepotezwa au ilibadilishwa katika harakati za kutafsiri. Aidha mfasiri huwa katika nafasi bora ya kuhakiki matini za kibibilia anapokuwa na uelewa wa historia yake hususan uandishi na tafsiri zake. Kutokana na historia ya Biblia na tafsiri yake, imebainika kuwa wafasiri wa Biblia hawakulipa kipaumbele suala la aina za matini na uamilifu wa kimawasiliano bali walijishughulisha zaidi na masuala kama vile misimamo yao ya kithiolojia; historia na utamaduni wa LC na LL; masuala ya kiisimu kama vile lahaja na ukopaji na mitazamo ya kifalsafa kama vile ufeministi na usasaleo.

2.1 Fasili ya Matini za Kidini

Kietimolojia matini za kidini zinahusishwa na neno la Kilatini *Scriptura* linalomaanisha “andiko” na huelezwa kama matini ambayo ni msingi wa maisha fulani ya kidini na itikadi zake (tazama utangulizi). Matini za kidini hutumika kutoa maana na lengo katika maisha, kuibua uhusiano wa kina na Mungu, kuwasilisha kweli za kidini, kuhalalisha uzoefu wa kidini, kuunganisha jamii, na kuelekeza maisha ya kidini ya kibinafsi na ya jamii. Aidha matini ya kidini huwasilisha mapokeo na maadili ya kidini na hujumlisha kanuni zinazodhibiti hali ya kimwili, kiakili, kiroho na kijamii ya wafuasi wa dini fulani au vipengele muhimu vya kihistoria vya dini fulani.

Tunahoji kuwa si kila matini ya kidini inaweza kuchukuliwa kuwa “takatifu” kwa kuwa matini takatifu ni zile zinaaminiwa kuwa zimetokana na Mungu au waandishi walioongozwa na Mungu hivyo matini nyingine za kidini ni masimulizi kuhusu mada, mapokeo, au watu mashuhuri wa dini fulani na haziwezi kuchukuliwa kuwa takatifu. Istilahi muhimu inayohusishwa na matini ya kidini ni ‘orodha ya matini za kidini.’ (canon). Hii ni istilahi ambayo hurejelea mkusanyiko wa matini usiobadilika na unaokubaliwa na wafuasi wa dhehebu fulani kama kanuni ya imani. Baadhi ya mifano ya matini ya kidini ni kama vile:

Dini	Matini
Judaism	Tanakh (Biblia ya Kiyahudi)
Sikhism	Guru Granth Sahib
Uislamu	Qur'ani
Hinduism	Vedas
Confucianism	The Five Classics
Buddhism	Tipitaka
Ukristo	Biblia

Yafaa kuzingatia kuwa yamkini kila dini ina madhehebu kadha yenye ainatofauti za matini ya kidini (mathalan tafsiri tofauti za Biblia na nyimbo dini tofauti miongoni mwa Wakristo) hivyo fasili ya matini ya kidini inahusisha msambao mkubwa wa vitini.

2.2 Chimbuka la Dini ya Kikristo

Wasomi wa Biblia wanahoji kuwa dini ya Kiyahudi iliweka msingi wa dini ya Kikristo kwa kuwa Wakristo wa kwanza walikuwa Wayahudi katika eneo la Palestina. Ukristo ulianza wakati Yesu Mnazareti alipoanza kuishi takriban miaka elfu mbili iliyopita katika kipindi kijulikanacho kama KK (Kabla ya Kristo) wakati wa utawala wa Warumi. Umoja wa kisiasa na mfumo bia wa kisheria ambao Warumi walijifunza kutoka kwa Wayunani vilitoa mazingira bora ya Ukristo kuimarika na kuanza kuenea ulimwenguni.

Aidha ueneaji wa Ukristo kwa kasi ulichochea na amani iliyohifadhiwa na jeshi la Rumi pamoja na kuongoka kwa baadhi ya wanajeshi na viongozi. Baada ya Yesu kuzaliwa aliishi miaka thelathini ya ukimya kisha akahubiri na kufanya miujiza hadharani kwa kipindi cha mwaka mmoja kabla ya kusulubishwa. Nchini Syria katika mji wa Antioch ndipo wafuasi wa Yesu kwa mara ya kwanza waliitwa Wakristo kwa kuwa aghalabu walizungumza kuhusu Kristo (mtiwa mafuta). Baada ya Kifo cha Yesu katika mwaka wa 31 BK (Baada ya Kristo) Ukristo ulianza kuenea kwa kasi zaidi kuliko alipokuwa hai. Utawala wa Warumi uliwafanya watawaliwa kupoteza imani na miungu yao ambayo waliona ilishindwa kuwalinda dhidi ya Warumi hivyo kukawa na mwanya wa kiroho uliotoshelezwa na Ukristo. (Cairns, 1996, Edwards, 1997, Gonz'alez 2010). Wakristo wa kwanza walizingatia Agano la Kale (tangu sasa

AK) kama kanuni ya imani yao. Agano la Kale liliandikwa kwa lugha ya Kiebrania na Kiaramai (ambayo ndiyo lugha iliyozungumzwa na Yesu) kabla ya kutafsiriwa kwa mara ya kwanza kwa Kiyunani, tafsiri ijulikanayo kama *Septuagint* (tangu sasa LXX) katika karne ya pili KK na wasomi sabini wa Kiyahudi.

Ubeberu wa lugha ya Kiyunani kwa mujibu wa Kerber (2016) uliwashawishi waandishi wa Agano Jipya (tangu sasa AJ) kuandika kwa Kiyunani na Ukristo ulipoenea hadi sehemu za magharibi mwa Ufalme wa Warumi katika karne ya kwanza baada ya Kristo wafasiri wa Biblia walianza kufasiri kwa lugha ya Kilatini ili kuwafikia Wakristo ambao hawangeelewa Kiyunani kilichotumika katika LXX na AJ.

2.3 Ulimwengu wa Biblia

Sehemu kubwa ya historia ya Biblia ilifanyika katika nchi ya Palestina. Hili ni eneo ambalo Waisraeli waliamia kwa mara ya kwanza katika karne ya 13 KK baada ya kutoka utumwani nchini Misri. Eneo hili lilijulikana kwanza kama Kanani lakini jina lake na mipaka yake vilibadilika mara kadha katika karne zilizofuata. Nchi ya Israeli iligawanyika katika falme mbili (Israeli na Juda) baada ya kifo cha mfalme Suleimani, kisha baadaye Warumi wakaligawanya katika majimbo kadha, mathalan Judea na Galilayo. Chimbuko la neno *Palestine* kwa mujibu wa Keene (2002) ni Wafilisti ambao waliamia katika Ukanda wa Gaza yamkini wakati mmoja na Waisraeli chini ya uongozi wa Yoshua.

Eneo la Palestina lina maziwa mawili na mto mmoja: ziwa Galilayo, bahari ya Dead Sea na Mto Yordani ambao chanzo chake ni milima ya Lebanon. Katika AJ Ziwa Galilayo hujulikana pia kama Genesareti au Tiberio. Aidha kuna mlima kama vile Karmeli na Hermon na mabonde (mathalan ‘Megiddo’ na ‘Jezreel’) ambavyo vilikuwa muhimu sana kwa shughuli za kivita na kibiashara. Eneo la pwani ya Palestina lilikaliwa kwa muda mrefu na Wafilisti ambao walikuwa na uwezo mkubwa wa kijeshi wakilinganishwa na Waisraeli. Baadhi ya maeneo mengine muhimu katika jiografia ya Palestina ni Bonde la Jordan ambalo limefika hadi Afrika Mashariki, milima ya Samaria na Judea, eneo lenye miinuko yenye rotuba la ‘Transjordan’ na vilima vya Shephelah karibu na upwa wa pwani.

Hali ya anga ya Palestina ni yenye joto jingi (hadi nyuzi 40) katika upwa wa pwani ya Dead Sea na baridi kali hususan katika majira ya baridi na katika eneo la Upper Galilee. Hali kadhalika kulikuwa na misimu miwili ya mvua katika maeneo yenye miinuko na majira ya ukame kati ya mwezi Juni na September. Wakazi wa maeneo kame walitegemea kwa wingi maji ya visima. Baadhi ya miti iliyopatikana katika eneo hilo ni kama vile ‘acacia’ (iliyotumiwa na Waisraeli kujenga Sanduku la Agano na Hekalu), mialoni, mikalitusi, misonobari, mipopla, miwilo, seda na ‘oleanders’. Miti ya matunda iliyokuzwa ilikuwa milozi; ambayo ilikuwa muhimu kwa mafuta na mbegu; mitende na minazi ambayo ilitumiwa kama ishara ya ushindi, neema na unyofu katika AK. Pia kulikuwa na maua ainati (ambayo Yesu aliyaita “mayungiyungiya bondeni”) kama vile ‘crocuses’, mipopi, ‘anemones’, ‘crown’ ‘marguerites’, nasisa, na ‘cyclamens’. Pamoja na mimea hii Waisraeli walikuza mimea iliyotumiwa ama kama dawa au vikolezi, mathalan, vitunguu saumu, hisopo, haradali, anise, ‘cumin’, ‘dill’ na minanaa.

2.3.1 Ndoa na Familia za Wayahudi

Ndoa za Wayahudi zilikuwa za mitara. Ibrahimu, mwanzilishi wa taifa la Wayahudi, alikuwa na wake wawili. Mitara iliendelea hadi wakati ambapo mfumo wa utawala wa kifalme ulipoanza kuwahimiza Waisraeli kuoa mke mmoja. Mume na mke walikuwa na majukumu tofauti. Baba aliwajibikia mahitaji yote ya familia naye mama alijishughulisha na usimamizi wa masuala ya nyumbani. Mume alitambuliwa kama mwakilishi wa Mungu na alitarajiwa kuhakikisha kuwa watoto wana nidhamu bila kuwadhulumu. Torati iliruhusu kuuawa kwa watoto wakaidi. Wanawake huwakuruhusiwa kurithi mali ya familia isipokuwa wale wasio na ndugu wa kiume. Mzaliwa wa kwanza wa kiume alipewa urithi wa familia maradufu.

Ndoa za nyakati za Biblia zilipangwa na wazazi na ukoo na aghalabu mabinamu waliozwa. Kufikia nyakati za AJ sherehe ya arusi ilikuwa ikifanyika kwa awamu mbili: kutia sahihi mkataba mbele ya mashahidi wawili, kisha bwana arusi alimchukua mkewe kutoka kwao na kumpeleka kwake. Familia zote mbili zilitoa mahari ambayo yangekuwa pesa, mali, ardhi au watumwa.

2.3.2 Elimu ya Wayahudi

Kabla ya enzi za AJ elimu ya Wayahudi ilipokelewa nyumbani. Baadaye wavulana walihudhuria masomo ya kidini katika masinagogi ambako walifunzwa na walimu wa kidini (*rabbi*) na elimu ya wasichana iliendelea nyumbani chini ya uongozi wa mama. Wanafunzi walifunzwa kwa njia ya masimulizi ya kimapokeo kwa kuhimizwa kuyakariri na kuyaweka moyoni. Aghalabu elimu ya Wayahudi ilisisitiza uhawilishaji wa imani na mapokeo ya kidini kupitia kwa familia.

Talmu (akinukuliwa na Keene, 2002) anadai kwamba kulikuwa na masinagogi 480 yenye shule jijini Jerusalem pekee yake. Walimu hawakulipwa ujira wowote ila walijipatia riziki kwa kutumia ujuzi wa kazi za mikono. Mathalan, Mtume Paulo alijipatia riziki kwa kutengeneza na kuuza hema.

2.3.3 Vyakula na Vinywaji

Vyakula na vinywaji vilikuwa kiungo muhimu cha maisha ya kijamii na kidini ya wenyeji wa eneo la Palestina. Kwa kawaida, kula na kufunga ni masuala muhimu katika dini ya Wayahudi na Ukristo. Aidha sherehe ya Pasaka hususan miongoni mwa Wakristo ni ushirika muhimu wa kula pamoja.

Kilimo cha Waisraeli kilikuwa cha mashamba madogo madogo kwa nia ya kukidhi mahitaji ya vyakula ya familia. Baadhi ya matatizo yaliyokabili kilimo cha Waisraeli ni ukosefu wa mvua ya kutosha, ukame, uvamizi wa nzige na wadudu wengine mashambani na ama uvamizi au uporaji kutoka kwa majeshi ya maadui.

Nafaka kama vile ngano na shayiri vilikuwa vyakula muhimu kwa watu wa Israeli na vyote vilitumiwa katika kuoka mikate na keki. Unga wa shayiri, ulitumiwa na maskini na ule wa ngano ulitumiwa na matajiri. Kutokana na mapokeo ya Wayahudi yanayodai kuwa Kanani ilikuwa nchi “iliyojaa maziwa na asali” tunadokeza kuwa maziwa na asali vilikuwa vyakula muhimu kwao kwa kuwa yamkini walivitumia kila siku. Asali ilikuwa muhimu kuliko maziwa hususan kwa kuwa ilikuwa kikolezi cha mikate na keki.

Aina za mboga zilizokuzwa Palestina zilikuwa chache yamkini kutokana na hali ya ukame. Maharagwe na dengu ndizo aina za mboga zilizokuwa kwa wingi. Baadhi ya matunda muhimu kwa Waisraeli yalikuwa zeituni(ambazo ziliwapa mafuta) na zabibu, ambazo zililiwa au kutumiwa katika kutengeneza mvinyo. Tinizilikuwa muhimu kwa chakula na matibabu. Aina nyingine za nafaka zilizopatikana Palestina ni lozi na ‘pistachios.’

Nyama ilikuwa chakula cha sherehe maalum kama vile harusi au chakula cha kuwakaribisha wageni muhimu nyumbani (mathalan Ibrahimu alipowachinjia malaika ndama aliyenona na katika sherehe ya kumkaribisha mwana mpotevu nyumbani). Kutokana na ushahidi wa matumizi ya mara kadha ya samaki katika vitabu vya Injili imedokezwa kuwa Waisraeli walikula samaki kwa wingi kuliko nyama. Baadhi ya mifano ni kama vile muujiza wa Yesu kuwalisha watu elfu tano kwa samaki na mikate na Yesu mwenyewe aliposhiriki staftahi ya samaki pamoja na wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake.

2.3.4 Amali za Wapalestina

Katika Palestina ya karne ya kwanza amali muhimu zaidi zilikuwa kilimo na uvuvi hususan kwenye Ziwa Galilayo. Baadhi ya Wapalestina waliyatumikia majeshi yaliyowatawala kama watumwa. Familia nyingi zilitegemea ufugaji na kilimo cha mashamba madogo madogo kukidhi mahitaji yao. Wanaume walijishughulisha na kilimo na biashara huku wanawake wakijishughulisha na masuala ya nyumbani na kufuma vitambaa na mikeka ili kuchangia kipato cha familia. Wazazi waliwafunza watoto wao amali zao ili kuwawezesha kuifaa familia na kujitegemea.

Baadhi ya mimea iliyokuzwa Palestina ilikuwa zabibu, ngano, kitani na matunda. Zabibu zilikuwa zikivunwa kati ya Septemba na Novemba, kitani kati ya Machi na Aprili, ngano kati ya Mei na Juni na matunda yalivunwa mwezi Agosti au Septemba. Mifugo iliyofugwa ilikuwa kondoo, mbuzi, ng’ombe na punda. Wakulima wa Kiyahudi hawakufuga nguruwe kwa sababu imani yao ilifundisha kuwa nguruwe ni najisi. Punda walitumiwa kubeba mizigo mizito, mafahali katika kulima na kondoo walifugwa kwa ajili ya sufu. Aidha fahali na kondoo wanalichinjwa wakati wa sherehe maalum. Kazi ya uchungaji wa kondoo ilifanywa usiku na mchana. Zizi la kondoo lilizingiriwa na kuta za mawe na ilimlazimu mchungaji kulala langoni ili

kuwalinda kutokana na wezi na uvamizi wa wanyama. Aghalabu wavuvi walilazimika kushirikiana katika kuvuta nyavu zilizojaa samaki, kuhifadhi samaki kwa kuwatia chumvi na kuwakausha, kuwauza sokoni na kukarabati nyavu na vyombo ili vitumike tena.

Mahitaji ya amali ya wanaume walifanywa kuwa magumu zaidi kutokana na suala la kodi aina mbalimbali walizolipa. Wanawake hawakuhitajika kulipa kodi yoyote. Wanaume walihitajika kulipa nusu shekeli kila mwaka ili kugharamia shughuli za Hekalu. Aidha walilipa kodi kwa watawala wa Herodia na Rumi. Kutokana na hali hii wafanyakazi walihisi kunyanyaswa na wakati mwingine walijaribu kuasi dhidi ya mamlaka yaliyowatoza ushuru. Umaskini na majukumu ya ushuru viliwalazimu watu wengi kufanya kazi hadi pale ukongwe ulipowafanya kushindwa kuendelea kufanya kazi.

2.3.5 Maisha Vijijini na Mijini

Kwa muda mrefu wa historia ya Israeli maisha yalikuwa ya kilimo vijijini kabla ya watu kuanza kuhamia mijini kwa kuhofia usalama wao. Kufikia wakati wa kuzaliwa kwa Yesu miji ya eneo la Palestina ilikuwa imepiga hatua kubwa za kimaendeleo chini ya himaya za Wayunani na Warumi. Katika nyakati za Biblia vijiji havikuzingirwa kwa kuta kama vile miji. Hali kadhalika miji ilijengwa karibu na vyanzo vya maji, hivyo ilikuwa salama kuliko vijiji. Kwa mujibu wa Keene, utafiti wa wanaakiolojia umeonyesha kuwa kufikia mwaka 6000 KK watu walifanya kilimo ndani na kando kando ya mji wa Jericho. Yamkini wanavijiji waliishi katika mahema kwa sababu iliwalazimu kuishi maisha ya kuhamahama kadiri majira yalivyobadilika. Mafuta yaliyotokana namizeituni yalitumiwa kwa matibabu, upishi na kuwasha taa wakati wa usiku.

Miji ya kwanza ilijengwa takriban mwaka wa 4000 KK kutokana na hitaji la wakazi kujilinda dhidi ya maadui. Ijapokuwa watu wengi waliendelea kuishi vijijini kwa muda mrefu, mara kwa mara waliamia mjini kutokana na tisho la uvamizi na hali mbaya ya hewa. Lango la kuingia mjini lilikuwa jembamba na lenye ulinzi mkali. Shughuli muhimu kama vile biashara, shughuli za kisheria na kesi zilifanyika ndani karibu la lango hili. Mathalan, hapa ndipo Ruthu aliozwa kwa Boaz na jamaa wa karibu wa Ruthu alimkabidhi Boaz mahari. Miji ilikuwa na majengo ya ghorofa na barabara nyembamba. Warumi walijenga mitaro ya kupitisha maji safi hadi mijini na kwenye mabafu ya umma. Aidha kulikuwa na mitaro ya kupitisha maji machafu. Mfalme Herode

alipojenga miji ya Samaria na Kaisaria alitumia ramani ya Kirumi yenye barabara moja kuu (iliyounganishwa na nyingine ndogondogo) iliyopita katikati mwa jiji na nyumba zilizengwa katika makundi ya nyumba nne nne.

2.3.6 Usafiri katika Palestina

Usafiri kwa njia ya miguu ndio uliotumiwa na watu wengi zaidi wakati wa Biblia. Hata hivyo kulikuwepo usafiri kwa ngamia, punda na meli. Kufikia wakati wa Warumi mfumo wa usafiri kwa njia ya barabara ulikuwa umerahishishwa mno. Wakati wa AK kulikuwa na barabara chache sana katika eneo la Palestina. Huku mataifa ya kibaharia kama vile Misri na 'Phoenicia' yakitumia meli kwa usafiri, aghalabu Waisraeli waisafiri ardhini kwa kuwa waliogopa usafiri wa maji. Mathalan, safari za Ibrahimu kwenda Kanani, Yakobo kwenda Misri, Waisraeli katika jangwa la Sinai na Paulo kwenda maeneo tofauti kuhubiri injili zilikuwa za ardhini. Katika AK yamkini ni wakati wa mfalme Suleimani tu ndipo meli zilitumiwa kwa usafiri wa kibiashara na kwa msaada wa mfalme Hiram wa Tiro kwasababu Waisraeli hawakuwa na ujuzi wa ubaharia.

Wakati wa AJ usafiri kuingia na kutoka Israeli ulikuwa umeimarishwa na Warumi hivi kwamba matajiri wangetumia magari yaliyokokotwa kwa farasi. Warumi walijenga barabara hizo katika maeneo ambayo walidhani kuwa yalikuwa muhimu kwa kusafirisha mizigo na majeshi yao. Katika sehemu nyingine barabara hazikuwepo na kule ambako zilikuwepo zilikuwa nyembamba mno kiasi cha kumwezesha mtu mmoja tu kupita. Kisa cha Msamaria Mwema kinaakisi matatizo yaliyohusishwa na usafiri katika barabara hizi. Punda ndiye aliyekuwa mnyama wa kwanza kutumiwa kwa usafiri kabla ya farasi na ngamia. Farasi walitumiwa zaidi katika vita wakati wa AK kabla ya kuanza kutumiwa kwa wingi katika usafiri wa kawaida wakati wa AJ.

Katika nyakati za Biblia wafanyabiashara walisafiri mwendo mrefu kwa msafara ili kujilinda dhidi ya wavamizi na majangili. Kulikuwa na njia maalum katika Palestina (kati ya Bahari Mediterranean na Jangwa la Shamu) zilizofuatwa na misafara ya wafanyabiashara. Wasafiri waliosafiri kati ya Mesopotamia na Arabia, Misri na maeneo mengi ya Afrika walipitia katika eneo hili la Palestina lenye upana usiozidi kilomita 120. Miji muhimu ilijengwa katika njia hii na wasafiri walipoipitia walitozwa kodi na wenyeji.

2.3.7 Sherehe na Siku Takatifu

Wayahudi walisherehekea siku ya Sabato kila wiki ili kumkumbuka Mungu kama muumba wa mbingu na nchi na vyote vilivyomo. Hali kadhalika waliadhimisha sherehe za kila mwaka kama vile sikukuu ya Pasaka na sherehe za kila mwaka za mavuno ili kumshukuru Mungu kwa wema aliowatendea. Waisraeli walizingatia sherehe hizi kama kiungo muhimu cha dini yao. Siku ya Sabato ndiyo iliyokuwa sherehe muhimu zaidi kuliko sherehe nyingine zote. Wanadamu wote na mifugo walihitajika kupumzika na kumwabudu Mungu. Kihistoria, siku ya Sabato iliwakumbusha jinsi Mungu alivyowakomboa kutoka utumwa wa miaka 430 nchini Misri. Hali kadhalika walikumbushwa kuwa kazi na pumziko na muhimu katika maisha ya mwanadamu.

Pasaka (ambayo pia inajulikana kama Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu) ndiyo sherehe ya kila mwaka iliyokuwa muhimu zaidi. Ilifanyika jioni ya tarehe 14 ya mwezi wa Nissan na kila familia ilimtoa kafara mwanakondoo ili kuadhimisha siku ambayo “Malaika wa Kifo” alipita juu ya kila nyumba ya Mwisraeli kabla ya kuwaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri. Kufikia wakati wa Yesu, Pasaka ilikuwa imekuwa sherehe muhimu zaidi ya mahujaji waliotoka pembe zote za himaya ya Warumi ili kuabudu katika Hekala la Yerusalemu. Sherehe nyingine muhimu za mahujaji zilikuwa Pentekote, aliyofanyika siku 50 baada ya Pasaka ili kuadhimisha mwisho wa mavuno na Sikukuu ya Vibanda (Sukket) iliyoadhimishwa mwanzoni mwa majira ya baridi wakati wa mavuno ya matunda. Waisraeli walitoa sadaka kutokana na mavuno yao na kuishi kwenye vibanda ili kukumbuka miaka 40 ya safari ya kupitia jangwa la Sinai wakielekea Kanani, Nchi ya Ahadi. Wayahudi na Wakristo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato wangali wanasherehekea Siku ya Sabato na Sikukuu ya Vibanda.

2.3.8 Hekalu

Kuwepo kwa hekalu katika mji wa Jerusalem kuliakisi uwepo wa Mungu miongoni mwa Waisraeli. Hekalu lilijengwa mahali pale pale mara tatu kabla ya kubomolewa kabisa na Warumi katika mwaka wa 70 KK. Ujenzi huu ulifanyika katika vipindi tofauti kati ya enzi za mfalme Suleimani katika karne ya 10 kabla ya Yesu na wakati wa mfalme Herode katika Karne ya kwanza Kabla ya Yesu. Hekalu zote tatu ziliwekwa wakfu kwa ibada ya Mungu. Mfalme Suleimani alijenga hekalu la kwanza kwenye mlima wa mashariki mwa mji wa Yerusalemu.

Lilikuwa na umbo la mstatili na sehemu mbili kuu, Patakatifu na Patakatifu Mno. Kuta zake zilipambwa kwa dhahabu na pale Patakatifu Mno palipambwa kwa dhahabu safi. Ndani ya Patakatifu mno mlikuwa Sanduku la Angano. Hili hekalu la kwanza liliharibiwa na mfalme Nebukadneza wa Babeli kisha akawachukua Waisraeli mateka kwa miaka sabini.

Wayahudi waliorudi Israeli baada ya utumwa nchini Babeli walijenga hekalu la pili mahali pale ambapo la kwanza lilikuwa. Hili la pili lilikuwa dogo kuliko la Suleimani na lilikamilishwa mwaka wa 515 KK. Lilidumu kwa miaka zaidi ya 500 kabla ya kunajisiwa na mfalme Antiochus Epiphanes wa Nne aliyetawala kutoka 175 KK hadi 164 KK. Hatimaye liliwekwa wakfu upya katika sherehe ijulikanayo kama ‘Hanukkah’. Mpaka sasa sherehe hii huadhimishwa kila mwaka na Wayahudi.

Mfalme Herode hakulibomoa hekalu la pili, bali alilikarabati na kulifanya bora kuliko la Suleimani. Ili kuzuia maasi ya Wayahudi dhidi ya utawala wake alihakikisha kuwa ibada zao haziingiliwi. Kila sehemu ya hekalu ilipambwa kwa dhahabu safi. Kwenye lango la kuingia katika sehemu ya kwanza ya hekalu kuliandikwa ilani kwa lugha za Kilatini na Kiyunani kuwaonya wasio Wayahudi wasiingie wasije wakauawa. Wanawake walikuwa na sehemu yao maalum nje ya Patakatifu na wanaume waliruhusiwa kuingia Patakatifu hususan walipotoa kafara na wakati wa Sikukuu ya Vibanda. Kuhani mkuu aliingia Patakatifu Mno mara moja kwa mwaka wakati wa sherehe ya Siku ya Upatanisho (Yom Kippur).

2.3.9 Muziki na Sanaa

Tangu enzi za A.K, muziki na sanaa zimetumiwa kuboresha ibada, kuakisi hisia kuhusu mada za kibiblia na dhati ya imani za Wayahudi na Wakristo. Biblia ni hazina muhimu ya jumbe za kumuziki zilizotumiwa na Wayahudi (baada ya utumwa wao) na Wakristo wa zamani. Zaburi na Nyimbo zimetumiwa na Wayahudi na Wakristo kwa karne kadha kuboresha uimbaji katika ibada. Zaburi zinazopatikana katika AK ziliandikwa kwa madhumuni ya uimbaji wa waumini katika ibada na katika sherehe maalum kama vile Sikukuu ya Pasaka. Mtume Paulo katika waraka wake wa Waefeso ameonyesha kuwa Wakristo wa zamani waliimba ‘zaburi, tenzi na nyimbo za rohoni (Waefeso 5:19). Nyimbo dini nyingi za madhehebu ya Kikristo zimetungwa

kutokana na Biblia moja kwa moja. Aidha idadi kubwa ya nyimbo hizi ilitungwa kati ya karne za kumi na saba na kumi na tisa.

Wanakiolojia wanahoji kuwa kufikia karne ya tatu baada ya Kristo, uchoraji wa picha kutokana na masimulizi ya AK na AJ ulikuwa umeenea. Sanaa ilitumiwa kuchora na kufasiri masimulizi ya Biblia (mathalan, masimulizi ya Nuhu na Safina na Danieli katika tundu la simba yalitumiwa kuakisi wokovu na uponyaji kutoka kwa Yesu). Katika enzi za kati mitindo ya sanaa iliyotumiwa ilihimiza matumizi ya masimulizi na mifano ya vitu fulani kuwasilisha mada za Kikristo. Karne za 19 na 20 zilishuhudia maendeleo makubwa ya sanaa ya uchoraji na uchongaji iliyotumiwa kuwakilisha mada muhimu za Kikristo kama vile kuzaliwa kwa Yesu, wokovu na matumaini.

2.4 Uandishi wa Agano la Kale

Hapana shaka kuwa wasomi wa Biblia na Wakristo kwa jumla wanahoji kuwa chimbuko la Biblia ni Mungu na kwamba Biblia ni kitabu cha kihistoria kinachoungwa mkono na akiolojia, aidha kimejaribiwa kwa muda mrefu na kuonekana kuthibitisha madai yake. Hivyo huchukuliwa kama barua ya Mungu kwa wanadamu yenye mkusanyiko wa vitabu 66 vilivyoandikwa na waandishi 40 wakiongozwa na Mungu katika kipindi cha miaka 1500. Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa Agano la Kale liliandikwa kati ya 1660 KK na 400 KK katika lugha ya Kiebrania. Orodha ya kwanza ya AK ilijumuisha vitabu ishirini na viwili. Baadaye kuhani Ezra akisaidiwa na Walawi walioongoza Sinagogi walikamilisha uhariri na ukusanyaji wa vitabu vilivyosalia vya AK mwishoni mwa karne ya 5 KK. Baadhi ya waandishi wa AK ni kama vile Musa (aliyeandika vitabu vitano vya kwanza) Samweli, Jeremia, Ezekieli, Mfalme Daudi, Suleimani, Ruthu, Isaiah, Danieli na Malaki. (www.biblestudy.org/beginner/when-was-OT-written.html).

2.4.1 Miswada ya Agano la Kale

Utafiti kuhusu chimbuko la Biblia umeonyesha kuwa kuna zaidi ya miswada 1400 ya AK inayoshahibiana na iliyonakiliwa maeneo ya Mashariki ya Kati, Bahari Mediterranean na Bara Uropa. Miswada ya Dead Sea (The Dead Sea Scrolls) iliyogunduliwa nchini Israeli katika miaka ya 1940 na 1950 inatoa ithibati inayoweza kutegemewa kuhusu kuwasilishwa kwa Maandiko ya Kiyahudi (AK) karne kadha kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Shughuli ya kunakili Maandiko kutoka

kwa miswada asilia (master scrolls) ilifanywa kwa ustadi na umakinifu mkubwa na waandishi wa Kiyahudi ambao amali yao ilikuwa ni kuhifadhi usahihi wa vitabu vitakatifu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Waandishi hawa kwa mujibu wa Musau (2011) waliopewa mafunzo kuntu, walizingatia hesabu ya kila herufi, neno na aya wakivilinganisha na miswada asilia hivi kwamba kosa moja lingalihitaji nakala nzima kuharibiwa.

2.4.2 Tafsiri za Kwanza za Biblia

Baadhi ya tafsiri za kwanza za sheria za kidini za Wayahudi (Torah) zilifanywa katika nyakati za utumwa wa Wayahudi nchini Babeli wakati ambapo lugha ya Kiaramai ilifanywa lugha mawasiliano ya Wayahudi. Kwa mantiki hii tafsiri ya Kiaramai ya Biblia ya Kiebrania ijulikanayo kama *Targums* (jina jingine Tanakh) ilibuniwa ili kufikia idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiaramai ambao hawakuelewa maandiko wakati Torah iliposomwa katika masinagogi kwa Kiebrania. Hatimaye LXX ambayo ilikuwa tafsiri ya kwanza ya Kiyunani ya Biblia ya Kiebrania ilikubaliwa kama AK.

2.5 Uandishi wa Agano Jipya

AJ liliandikwa kwa Kiyunani ambayo ndiyo iliyokuwa lugha mawasiliano katika karne ya kwanza kati ya 46 BK na 100 BK. Waandishi wote wa AJ walikuwa Wayahudi isipokuwa Luka na watatu miongoni mwao (Mathayo, Petro na Yohana) walikuwa wanafunzi. Wasomi wa Biblia wanakubaliana kuhusu waandishi wa vitabu vya AJ na vitabu walivyoandika kama ifuatavyo:

Mwandishi	Kitabu
Yakobo	Yakobo
Yohana	Injili ya Yohana, 1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana, Ufunuo
Yuda	Yuda
Luka	Injili ya Luka, Matendo ya Mitume
Marko	Marko
Mathayo	Injili ya Mathayo
Paulo	Warumi, Wakorintho 1 na 2, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, Wathesalonike 1 na 2, Timotheo 1 na 2, Tito, Filemoni, (yamkini Waebrania pia)
Petro	1 Petro na 2 Petro. (www.bible-history.com/new-testament)

2.5.1 Tafsiri za Biblia Baada ya Mitume

Hadi karne ya tatu, lugha ya Kanisa la Rumi ilikuwa Kiyunani na ndiyo iliyokuwa lugha mawasiliano ya Wayahudi katika eneo la Palestina. Kwa hakika maandiko ya kwanza ya Kikristo yaliandikwa kwa lugha ya Kiyunani: Mathalan Barua ya Paulo kwa Warumi na barua ya Clement, askofu wa Rumi kwa Wakorintho. Miongo michache baada ya kifo cha Yesu idadi ya Wakristo iliongezeka katika mji wa Rumi (na maeneo mengine nchini Italy) ambapo lugha mawasiliano ilikuwa Kilatini na hatimaye wazungumzaji wa Kilatini wakawa wengi magharibi mwa Himaya ya Warumi.

Kutokana na kuenea kwa Ukristo katika maeneo ya magharibi mwa Himaya ya Warumi hitaji la kuandikwa kwa tafsiri za Kilatini za matini za Kibiblia liliongezeka ili kufikia hadhira ambayo haikuelewa Kiyunani cha AJ na LXX. Umaarufu wa Kilatini kama lugha mawasiliano ulienea hadi Afrika Kaskazini, Uhispania, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Luxembourg, Ubelgiji, Uswizi na Uholanzi. Kwa mujibu wa Kerber (2016) tafsiri za kwanza za Kilatini zijulikanazo kama *Old Latin* au *Vetus Latina* zilifanywa barani Afrika katika karne ya pili na watu binafsi ili kutumiwa katika jamii zao. *Vetus Latina* ni istilahi inayorejelea matini za Biblia ya Kilatini zilizotafsiriwa kutoka Kiyunani kuanzia karne ya pili. Matini hizi zina umuhimu mkubwa kwa historia ya Kanisa na tafsiri ya Biblia. Hatimaye tafsiri ya Kilatini ijulikanayo kama *Vulgate* ilifanywa kwa kipindi cha miaka zaidi ya ishirini (382-407) na mfasiri mashuhuri aliyejulikana kama Jerom. Ijapokuwa Jerom hakutafsiri Biblia nzima, kazi yake ilihaririwa na hatimaye matini zilizosalia kutafsiriwa na wafasiri wengine. Aidha tafsiri nyingine za Kilatini ziliendelea kuandikwa kati ya karne ya nne na mwishoni mwa Enzi za Kati.

Katika karne ya kumi na nne, John Wycliffe na wafuasi wake waliandika tafsiri ya kwanza ya Kiingereza ya AK na AJ. Hii ilitokana na msukumo wa wafasiri wa Biblia kuwasilisha ujumbe wa MC kwa lugha enyeji ya HL. Hatimaye kwa juhudi za miaka zaidi ya kumi (1518-1534) Martin Luther kwa msaada wa Philip Melancthon alifanikiwa kuandika tafsiri za kutoka Kiebrania hadi Kijerumani za AJ na AK. Hatimaye wasomi arobaini na saba wa Biblia kwa amri ya mfalme James walihariri tafsiri za kutoka Kiyunani hadi Kiingereza zilizofanywa na William Tyndale na katika mwaka wa 1611 wakachapisha tafsiri rasmi ya Kiingereza ya KJV (ijulikanayo pia kama Authorized Version).

2.5.2 Tafsiri za Kiingereza

Taafsiri ya Kwanza ya Biblia kutoka MC za Kiebrania na Kiyunani hadi Kiingereza ilifanywa kwa mara ya kwanza na msomi Mwingereza, William Tyndale (1494-1536). Tafsiri ya *Tyndale Bible* ndiyo iliyokuwa ya kwanza kuchapishwa hivyo ikawa kiunzu cha tafsiri nyingine za Kiingereza zilizofuata. Ushindani kati ya tafsiri za *Bishops Bible* na *Geneva Bible* ulimfanya Mfalme James wa Kwanza kuagiza mradi wa tafsiri ya ‘Authorized Version’ iliyochapishwa mwaka wa 1611. Tafsiri ya ‘The Revised Version’ ya mwaka wa 1881 ilikusudiwa kuisanifisha tafsiri ya ‘Authorized Version’ na tafsiri ya *Revised Standard Version (RSV)* ya 1952 ikaondoa ukale wake. Aidha ‘Jerusalem Bible’ inayotumiwa na Kanisa Katoliki ilichapishwa mwaka wa 1966 na ‘New English Bible’ iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1961 ilitafsiriwa upya na kuchapishwa mwaka wa 1989 kama *Revised English Bible*. Tafsiri nyingine muhimu hususan kwa wasomaji wa Kiprotestanti ni *Good News Bible* (1976) na *New Internaitonal Version (1978)*. Jumla ya tafsiri za Kiingereza za Biblia ama yote au matini zake kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni ni zaidi ya 900. Uelewa wa lugha ya Kiebrania kwa mujibu wa Jeffrey (2012) huwawezesha wafasiri wa Biblia za Kiingereza kuzingatia ulinganifu wa maana.

2.6 Biblia na Mageuzi

Mageuzi ni istilahi inayorejelea vuguvugu la kidini la karne za 15 na 16 lililosababisha kuanzishwa kwa Makanisa ya Kiprotestanti barani Uropa hususan *Lutheran* na *Presbyterian*. Chimbuko la Mageuzi lilikuwa kukubaliana na kutokubaliana kuhusu uelewa wa vipengele fulani vya matini za Biblia. Wanamageuzi mashuhuri kama vile Martin Luther, John Calvin na Ulrich Zwingli walikubaliana kuhusu umuhimu wa Biblia kama kanuni ya imani lakini uelewa wao wa Biblia ulitofautiana.

Wanamageuzi wote walikubaliana kueneza imani ya Kikristo kwa kuhubiuri na kufundisha Biblia, na kutojumuisha matini zijulikanazo kama *Apocrypha* katika Biblia. Huu ni mkusanyiko wa matini za Kiyahudi zilizo na uhusiano fulani na AK na AJ (mathalan *Tobit*, *Judith*, *1 Maccabees* na *2 Maccabees*) ambazo zimejumuishwa katika AK la Kanisa Katoliki na dhehebu la Eastern Orthodox Christians lakini hazipo katika Biblia za Kiprotestanti. Hali kadhalika walikubaliana kuwa MC ya Biblia ya Kiebrania na Kiyunani ni takatifu na mapokeo na mafundisho ya Kikristo sharti yaongozwe nayo. Vuguvugu hili lilishikilia kuwa sharti Maandiko

yawasilishwe kwa lugha enyeji za HL ili wenyeji wajisomee wenyewe bila msaada wa viongozi wa kidini. Vinginevyo tofauti za uelewa za wanamageuzi zilikitwa katika mitazamo tofauti ya ufasiri wa baadhi jumbe za AK na AJ (Taz. Keene, 2002).

2.7 Tafsiri za Kisasa za Biblia

Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa Biblia ndiyo matini iliyotafsiriwa zaidi ya nyingine zote. Hivyo upatikanaji wa Biblia nzima au sehemu yake kwa hadhira kubwa ulimwenguni na kwa lugha za kwanza umefanikishwa kwa kiasi kikubwa. Kufikia mwezi Septemba 2016 Biblia nzima ilikuwa imetafsiriwa kwa lugha 636, AJ katika lugha 1442 na matini za Kibiblia au masimulizi yake katika lugha nyingine 1145, kwa jumla Biblia nzima na matini zake zimetafsiriwa kwa lugha 3,223 (United Bible Society, 2016). Tafsiri zakisasa za Biblia ya Kiswahili ni SUV (1952, 1997) iliyochapishwa na Bible Society of Tanzania na Bible Society of Kenya na BHN (ambayo ni mshabaha wa tafsiri ya ‘Good News Bible’) iliyochapishwa mwaka wa 1995/ 2001 na Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Bibilia cha Kenya.

2.8 Tofauti za Kihistoria za Wafasiriwa Biblia

Nadharia ya tafsiri inaakisi mitazamo tofauti inayoweza kutumikizwa katika taaluma ya tafsiri, mathalan tafsiri sisisi, tafsiri kielimumitindo na tafsiri kimawasiliano. Kwa mantiki hii mbinu tofauti za kutafsiri Biblia zimetumika kwa kutegemea mtazamo wa kila mfasiri kutika kuwasilisha ujumbe wa MC ambao uliwasilishwa kwa Kiebrania na Kiyunani. Matokeo yamekuwa ni tafsiri tofauti zenye mitazamo tofauti kwa hadhira ya lugha moja. Kwa mfano, tafsiri za Kiingereza za King James Version, New Revised Standard Version na Modern Literal Version ni sisisi huku New American Standard Bible, New International Version na The Living Bible zikiwa tafsiri huru. Aidha tafsiri tofauti za Kiswahili zimeshawishiwa na tofauti za kiisimu na kifalsafa. Uhakiki wa tafsiri za Kiswahili umeonyesha kuwa SUV ni tafsiri sisisi na BHN ni tafsiri huru.

Utafiti umeonyesha kuwa kadiri wafasiri wanavyojitenga na tafsiri ya neno kwa neno ndivyo matini tafsiri zinasomeka kwa urahisi hususan mfasiri anapotumia umilisi wa kimawasiliano na uelewa wa utamaduni wa LL na LC kwa ustadi. Hata hivyo ukopaji wa maneno na misemo ya LC ni mbinu kubalifu ilmradi LL ifaidi kutokana navyo. Tunahoji kuwa mtazamo wa kieklektika

unaopendekezwa na Brunn (2013) ndiyo mbinu bora zaidi ya kukabiliana na tofauti za kiisimu na kifalsafa za wafasiri wa Biblia. Ni nadra tafsiri kuwa sisisi tupu au wazo kwa wazo tupu kwa kuwa nyingi zinaakisi matumizi ya mbinu hizi mbili kwa pamoja: neno kwa neno na wazo kwa wazo.

Hoja nyingine inayozua tofauti za tafsiri mbali na mitazamo tofauti ya kiisimu na kifalsafa ni mipaka ya kithiolojia. Baadhi ya tafsiri za Biblia zimekitwa katika msimamo fulani ya kithiolojia ya wafasiri. Mathalan, tafsiri ya Kiingereza ya ‘New World Translation’ (NWT) iliyofanywa na dhehebu la Jehova’s Witness (linalofundisha kuwa Yesu hana asili ya Uungu bali ni mwanadamu aliyeumbwa) inatumia maneno yanayoakisi ubinadamu wa Yesu pale ambapo tafsiri nyingine zinakisi Uungu wake. Aidha tafsiri za maneno ya Kiyunani na Kiebrania kama vile ‘YHWH’, *Kurios* na *Theos* zinaonyesha tofauti za kithiolojia kama ifuatavyo:

Istilahi	Tafsiri ya NWT	Tafsiri nyingine
‘YHWH’ (Kiebrania) Jehovah		Lord
<i>Kurios</i> (Kiyunani)	Jehovah	Lord
<i>Theos</i> (Kiyunani)	Jehovah/ au Elohim (SSBE)	God

Kwa mantiki hii katika tafsiri ya NWT neno *Jehovah* limeingizwa mahali pa neno *kurios* (*Lord*) mara 237 katika AJ na mara 6,979 katika AK badala ya “YHWH”(God), jumla ya mara 7,216. Hali kadhalika tofauti nyingine za tafsiri zimebainishwa kwa tafsiri zinazohimiza misimamo fulani katika maisha ya Ukristo. Kwa mfano tafsiri ya ‘Purified Translation of the Bible’ imetumia maneno ‘grape juice’ badala ya ‘wine’ ili kutetea hoja kuwa Wakristo hawastahili kunywa pombe.

2.9 Historia ya Biblia ya Kiswahili

Chimbuko la fasihi andishi ya Kiswahili katika herufi za Kilatini lilihusishwa na kazi za kiisimu za wamishenari wa Kikristo ambazo zilianzishwa katika miaka ya 1840 kwa kufasiri sehemu za Biblia kwa Kiswahili hususan kitabu cha Marko. Wafasiriwa kimishenari walitumia muda mwingi wa maisha yao kwa shughuli ya kutafsiri Biblia, kutalii Kiswahili na lugha enyeji nyingine kisha kutafsiri sehemu za Biblia, Maombi na Nyimbo Dini kwa lugha hizi enyeji. Uchapishaji wa Biblia nzima au matini zake na tafsiri ya riwaya ya Bunyan ijulikanayo kama

Pilgrims Progress from This World to That Which is to Come katika mwaka wa 1888, yaani *Msafiri*, ndizo zilikuwa kazi za kwanza za tafsiri kuchapishwa na kwa muda mrefu Biblia pekee yake ndiyo iliyokuwa matini tafsiri ambayo ingesomwa kwa lugha enyeji.

Mradi mpya wa kutafsiri Biblia katika Kiswahili ulianza mwishoni mwa utawala wa Wajerumani Afrika Mashariki. Kufikia mwongo wa kwanza wa karne ya Ishirini wamishenari wa Ki-Lutheran walitambua umuhimu wa kutumia lugha mawasiliano, Kiswahili, katika kuwasilisha ujumbe wa Biblia hivyo wakaanza kupanga mipango ya kufanikisha upatikanaji wa tafsiri ya Kiswahili. Mmishenari wa kwanza kutafsiri Biblia katika Kiswahili alikuwa Mmishenari wa Church Missionary Society (CMS); Ludwig Krapf, katikati ya karne ya kumi na tisa, kwa lahaja ya Kimvita. Krapf alikuwa mwasisi katika nyanja za isimu na tafsiri hususan za Kiswahili. Kwa mujibu wa Vilhanova (2006) tafsiri za Krapf za vitabu vya Injili na Kamusi ya kwanza ya Kiswahili aliyoiandika vilitoa mchango mkubwa kwa kazi za tafsiri za Bishop Steer na vilitumika kama msingi wa tafsiri za lugha nyingine enyeji, mathalan tafsiri ya Biblia ya Luganda ya George Pilkington's katika miaka ya 1890.

Miaka kadha baada ya tafsiri ya Kimvita, Askofu Edward Steere wa Universities' Mission to Central Africa (UMCA) alitafsiri Biblia kwa lahaja ya Kiunguja. Steer alianza kazi ya kutafsiri AJ katika mwaka wa 1874 baada ya kutawazwa kuwa Askofu wa Unguja. Alitafsiri na kuchapisha kwa Kiswahili matini za dini ya Kikristo na Biblia nzima katika mwaka wa 1891. Kufikia mwaka wa 1880 alikuwa ametafsiri AJ na katika mwaka wa 1882 akachapisha toleo lake jipya. Toleo la kwanza la tafsiri ya Kiswahili ya AJ lilichapisha nakala 5050 katika 1883 na zilisafirishwa kwa meli hadi Unguja. Aidha alitafsiri matini fulani za AK kama vile 1 Wafalme, 2 Wafalme na Isaya kabla ya kifo chake mwaka wa 1883.

Hata hivyo Karl Roehl na wamishenari wengine walihofia kuwa huenda watu wanaozungumza Kiswahili kama lugha ya pili hususan wakazi wa bara wasingeelewa tafsiri hizi mbili. Kwa mantiki hii wakaona haja ya kuandika tafsiri ambayo ingewafaa wamishenari na HL. Martin Klamroth, mmishenari wa Berlin Mission alipewa jukumu la mradi wa tafsiri bora ya Biblia ya Kiswahili. Baada ya kifo cha Klamroth katika mwaka wa 1918 Roehl n.w akapewa jukumu la kuhariri tafsiri yake na kuiandaa kwa uchapishaji.

Baada ya vita vya pili vya dunia Wajerumani walishurutishwa kuwacha koloni yao katika Afrika Mashariki kupitia kwa mkataba wa Versailles. Hata hivyo wamishenari wa Kijerumani waliruhusiwa kurejea Tanganyika baada ya 1925 na kuendelea na mradi wa tafsiri ya Biblia. Wakoloni wa Uingereza walianzisha mchakato wa usanifishaji na upangaji wa lugha ya Kiswahili katika mwaka wa 1925 kisha ukaendelezwa na kamati ya *Inter-Territorial Language Committee* iliyobuniwa mwaka wa 1930 na serikali za kikoloni za Tanganyika, Kenya, Unguja na Uganda. Tafsiri ya Kiswahili ya Roehl ambayo ilijepusha na maneno ya Kiarabu (Mathalan *Asli* na *fikra*) iliidhinishwa na *Inter-Territorial Language Committee* na kuchapishwa na shirika la Bible Society katika mwaka wa 1937. Juhudi za Roehl kuepuka kutumia maneno mkopo kutoka Kiarabu zilizua tofauti za kiisimu kati yake na washirika wake kwa upande mmoja na wamashenari wengine na wanaisimu (mathalan Canon Broomfield, ambaye alihoji kuwa maneno mkopo ya Kiarabu yamekuwa sehemu ya Kiswahili) hivyo mjadala kuhusu tafsiri ambayo ingehusisha wadau wote (SUV) ukaanzishwa. (Hunter: 2013).

Ni bayana kuwa historia ya Biblia ya Kiswahili imetawaliwa na matapo mawili ya wafasiri: Kimvita na Kiunguja. Kutokana na juhudi za serikali za Afrika Mashariki na mashirika ya kimishenari kama vile *British and Foreign Bible Society* (BFBS), *Universities' Mission to Central Africa* (UMCA) na *Church Missionary Society* (CMS), hatua za kwanza za kuchapisha tafsiri moja ya Kiswahili sanifu yenye kuunganisha matapo haya mawili zilionekana katika mwaka wa 1928. Wazo hili liliibuliwa na Kongomano la Usanifishaji wa Kiswahili lililofanyika jijini Dar es Salaam katika mwezi Oktoba mwaka wa 1925 na jingine la Mombasa katika mwezi Juni tarehe 3, 1928. Katika kikao cha wafasiri wa kimishenari jijini London wakiongozwa na E.W. Smoth (wa BFBS) iliamuliwa kuwa tafsiri ya Kiunguja ya Agano jipya itumike kama data ya kimsingi ya mradi mpya wa tafsiri ya AJ na ile ya Roel ambayo iliegemea Kibantu itumike kama data ya upili. Aidha tafsiri ya AK ya Roehl ilikubaliwa kama data ya msingi katika kutafsiri AK na zile za Kimvita na Kiunguja zilitumika kama data ya upili. Hatimaye wafasiri walikubaliana kujitenga na tafsiri ya Kimvita aliyoasisiwa na Krapf na wamishenari wenzake wa CMS kutoka pwani ya Kenya. Mradi wa tafsiri ya umoja ya Biblia ya Kiswahili uliongozwa na kanuni za tafsiri zilizobuniwa na shirika la BFBS.

Toleo la kwanza la tafsiri ya umoja lilitafsiriwa na Godfrey Dale (UMCA, Unguja) na kuhaririwa na G. Pittway na H.J. Butcher (CMS, Mombasa) kisha kuchapishwa na BFBS, jijini London mwaka wa 1934. Hata hivyo Roel alitofautiana na wafasiri wenzake kwa msingi kuwa ilikuwa na maneno mkopo mengi ya Kiarabu. Baada ya tofauti hii tafsiri ya Roehl iliyojumuishwa AJ na AK ilichapishwa katika mwaka wa 1937 na 1961 na Shirika la Whurtemberg Bible Society jijini Stuttgart, kabla ya kuchapishwa upya mwaka wa 1995. Tafsiri hii ilikamilishwa kwa msaada wa wenyeji wawili; Mchungaji Martin Ngamisya na Mwalimu Andrea Ndekeja. Baada ya Roel kujiondoa katika mradi wa tafsiri ya umoja Canon Hellier wa UMCA kwa msaada wa Paulo Kihampa na Canon Butcher wa CMS walihusishwa kama wafasiri wakuu na Richard Reusch wa Lutheran n.w kama mhariri. Kufikia mwaka wa 1949 matoleo ya muda ya Injili za Mathayo, Marko na Yohana pamoja na Zaburi yalichapishwa na shirika la CMS jijini Nairobi. Hatimaye toleo la kwanza la AJ la SUV lilichapishwa mwaka wa 1950 na AK mwaka wa 1952 na shirika la BFBS. Kwa mujibu wa Mojola (2000: 511) mradi wa tafsiri ya Biblia ya SUV uligharimu muda mrefu kwasababu ya tofauti za kibinafsi, kiusomi, kiimani na kithiolojia za wafasiri waliohusika.

Tunatambua kuwa wamishenari wa Kanisa Katoliki pia wametoa mchango muhimu katika historia ya Biblia ya Kiswahili. Vitabu Kumbukumbu vijulikanavyo kama *Apocrypha* vilitafsiriwa na D.V. Perrot na kuingizwa katika SUV kisha kuchapishwa mwaka wa 1967 kama tafsiri mpya ya Kanisa Katoliki. Tafsiri nyingine iliyofanywa na wafasiri wa Kanisa Katoliki ni ile ya AJ iliyofanywa na Benedictine Fathers na kuchapishwa mwaka wa 1986.

Tafsiri ya SUV kwa mujibu wa Mojola (2000:521) imekubaliwa kwa muda mrefu na wasomaji na wafasiri na mshabaha wake wa Kiingereza ni KJV. Hii ndiyo tafsiri ya kwanza isiyoegemea dhehebu lolote kabla ya tafsiri ya BHN iliyokuwa mradi wa makanisa yote. BHN ndiyo tafsiri ya kwanza ya Kiswahili iliyohusisha wenyeji wa Afrika Mashariki pekee. Mradi huu ulianza mwaka wa 1973 na ulishirikisha wafasiri kutoka madhehebu kadha: Peter Renju (Katoliki) Cosmas Haule (Katoliki), Jared Mwanjala (Angilikana), Amon Mahara (Lutheran), Amon Oendo (Waadventista wa Sabato), Douglas Waruta (Baptist), David Mhina (Anglikana) na Leonidas Kalugila (Lutheran).

AJ la tafsiri ya Biblia Habari Njema lilichapishwa mwaka wa 1977 na kupokelewa vyema na wasomaji. Hatimaye kupitia kwa juhudi za muda mrefu BHN ilichapishwa na kuanzishwa rasmi nchini Kenya na Tanzania tarehe 24 Machi mwaka wa 1996. Tafsiri ya BHN ni ya mtazamo wa ulinganifu wa maana wala si tafsiri sisisi kama SUV.

2.10 Biblia ya Kikristo na Apokrifa

Kietimolojia, neno *Apokrifa* ni tafsiri ya neno la Kiyunani lenye maana ya “vitu fiche” na hurejelea matini ambazo zimewekwa katikati ya AK na AJ katika Biblia kadha za Kikristo hususan zile zilizochapishwa na Kanisa la Rumi. Ijapokuwa matini hizi si sehemu ya Tanakh (Biblia ya Kiyahudi) baadhi yavyo viliingizwa katika LXX na tafsiri ya Vulgate. Kwa mujibu wa Keene (2002) vitabu vya *Apokrifa* vilijumwishwa katika Biblia na Kanisa Katoliki lakini baadaye katika nyakati za Mageuzi ya Kanisa la England, kanisa liliviondoa katika Biblia kwa kuwa vilihusishwa na mafundisho potofu kuhusu hukumu na wokovu. Kwa jumla, *Apocrypha* inajumuisha vitabu saba vya kihistoria: *1 Esdras na 2 Esdras, Tobit, Judith, Wisdom of Solomon, Ecclesiasticus, Baruch, 1 Maccabees na 2 Maccabees*.

2.11 Biblia na Ufeministi

Tangu miaka ya 1960 kumekuwa na mjadala mkali kuhusu iwapo ni Biblia imechangia pakubwa taasubi ya kiume au ni mifumo ya jamii za Kiyahudi na Kikristo. Elimu na mafunzo bora kwa wanawake vimeimarisha hadhi na nafasi yao katika jamii. Kwa mantiki hii wanawake wengi wamedara chukulizi kuwa mwanamke amedhalilishwa katika Biblia. Grimke (akinukuliwa na Keene,2002) anahoji kuwa ufasiri wa Biblia ulikusudiwa kuwadhalilisha wanawake. Katika mwaka wa 1895 makala ya *The Womens Bible* yalichapishwa kupinga wazo kuwa utamaduni na mafundisho ya Biblia vinastahili kutumikizwa katika maisha ya sasa bila kudarwa. Hata hivyo, baadhi ya wafeministi wanahoji kuwa suala la taasubi ya kiume katika Biblia katu haliwezi likarekebishika na hivyo wamejitenga na jamii za Wayahudi na Wakristo. Aidha kuna wanawake wengi ambao wameendelea kutambua mamlaka ya Biblia na wanatekeleza majukumu muhimu katika makanisa na masinagogi. Mtazamo wa kifeministi umekuwa ukitetea tafsiri za Biblia zinazozingatia usawa kati ya wanawake na wanaume na matumizi ya jinsia zote mbili katika kumrejelea Mungu.

2.12 Biblia na Usasaleo

Usasaleo ni mtazamo wa kifalsafa wa karne ya 20 na 21 unaodara mamlaka ya Biblia kwa kudai kuwa mwanadamu ana uhuru wa kuishi atakavyo na kuwa mfuasi wa dini atakayo. Wanausasaleo wanahoji kuwa Biblia ni kitabu cha kawaida na kwamba mafundisho yake hayawezi yakachukuliwa kama ukweli katika ulimwengu wa leo ambao umebadilika.

Mtazamo wa usasaleo kuhusu Biblia umekitwa katika kanuni tatu: lugha ni chombo muhimu katika mwonoulimwengu wetu; misingi ya kitamaduni na kimaadili ya Biblia vimefanya ukweli wake kufichika kwa ulimwengu wa leo; kutoamini yote yaliyosimuliwa katika masimulizi makuu kama vile Biblia ni jambo linalokubalika.

2.13 Muhtasari

Tafsiri za Biblia kwa lugha ya Kiswahili ni nyingi kuliko lugha nyingine yoyote enyeji katika Afrika Mashariki. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha mawasiliano katika kanda hii hivyo ina ushawishi mkubwa kwa wafasiri na wasomaji . Tafsiri tano muhimu za Biblia ya Kiswahili ni: Kiunguja (1891), Kimvita (1914), Roehl (1937), SUV (1952) na BHN (1996). Hatua zilizopigwa katika tafsiri ya Biblia ya Kiswahili na matini zake zinaakisi juhudi za wafasiri katika kuhakikisha kuwa ML inatoa ujumbe wa jumla usiofungamana na utamaduni wa MC ili kufikia matarajio na mahitaji ya HL.

Baada ya uchanganuzi huu wa historia ya Biblia na tafsiri yake tunaweza kuhoji kuwa dhima ya historia hii ni kumsaidia mfasiri wa matini za kibiblia kuwa katika nafasi bora ya kutekeleza kwa ufanisi shughuli yake ya kufasiri kwa kuwa ni kiungo chake muhimu. Hoja ambayo tunataka kulisitiza hapa ni kuwa stadi yetu imeonyesha kuwa wafasiri wengi wa matini za kibiblia hawakuzingatia suala la aina za matini na uamilifu wa kimawasiliano kama kigezo kinachoshawishi mbinu za tafsiri. Kwa mantiki hii, utafiti wetu ulilenga kuziba mwanya huu kwa kuchunguza nafasi ya simulizi, matini elekezi na shairi katika kushawishi mbinu za tafsiri.

SURA YA TATU MATINI ZA BIBLIA

3.0 Utangulizi

Tumetaja kuwa matini za Biblia ziliandikiwa katika nyakati tofauti na waandishi tofauti ambao aghalabu hawakuzingatia suala la aina za matini kama kigezo kinachoshawishi mbinu za tafsiri. Wasomi wa Biblia wanadai kuwa hakuna mswada asilia hata mmoja wa Biblia uliohifadhiwa, hivyo wamejaribu kutafuta matini ya zamani zaidi inayoweza kutegemewa. Katika sura hii tumetathmini mbinu za uhakiki wa matini za kibiblia, uasili wa MC ya Biblia na vipengele vya aina za matini hususan mitindo ambayo yamkini ni muhimu katika kushawishi mbinu za tafsiri. Tumehoji kuwa uhakiki wa MC ya Biblia humwezesha mfasiri kuepuka kuingiza chukulizi mpya katika ML na kutambua nduni za utanzu anaoushughulikia kwa kuwa ndizo huakisi uamilifu wa kimawasiliano wa MC. Hali kadhalika vipengele hivi humwezesha mfasiri kufikia mahitimisho kadhaa ambayo humsaidia kuchagua aina ya tafsiri inayofaa zaidi kwa matini anayoishughulikia.

3.1 Matini Chanzi za Agano la Kale

Matini asilia zaidi ya Kiebrania ambayo ndiyo chimbuko la tafsiri nyingine za Kiyahudi ni ile ijulikanayo kama *Masoretic Version*. Wa-Masorete (500-1000BC) walikuwa wasomi wa Kiyahudi walioongeza vokali katika matini ya Kiebrania ambayo iliandikwa kwa konsonanti tupu kisha wakahifadhi utakatifu wake kwa kuibana kwa alama maalum juu na chini ya mistari. Kwa mujibu wa Keene (2002) ubora wa kazi ya matini ya Wa-Masorete huweza kupimwa kwa kuilinganisha na miswada ya *Dead Sea Scrolls* ambayo imekuwepo takriban miaka 1000 kabla ya tafsiri yoyote ya Kiebrania, hivyo ndiyo sahihi zaidi.

3.2 Matini Chanzi za Agano Jipya

Wasomi wa Biblia wanahoji kuwa kuna maelfu ya miswada ya Kiyunani ya AJ. Miswada ya zamani zaidi iliyokamilika ni ile iliyoandikwa kati ya Karne ya nne na karne ya tano A.D. Miswada mingine ilipatikana vipande tofauti na kufungwa pamoja kama vitabu (codices). Maandishi ya matini hizi hayakuzingatia hijai wala uakifishaji. Maandiko asilia yaliyo muhimu sana ni yale ya *Codex Sinaiticus* (yaliyoandikwa kwa herufi kubwa pekee) na *Codex Vaticanus*. Aidha mswada wa *Codex Bezae* una matini za Kiyunani na Kilatini za Injili na Matendo ya

Mitume. Mswada unaoaminika kuwa wa zamani zaidi (135 AD) ni sehemu fupi ya Yohana 18 iliyogunduliwa nchini Misri na kuchapishwa mwaka wa 1935.

3.3 Mbinu za Uhakiki wa Matini za Kibiblia

Biblia ni hazina kuu ya aina za matini za kifasihi zilizokusanywa na kuwa diwani ambamo ndani yake mna AK na AJ. Hivyo mkusanyiko huu wa matini za kifasihi huweza kuhakikiwa kwa kutumikiza mbinu za uhakiki za matini yoyote ya kifasihi. Uhakiki wa kibiblia umekitwa katika kutumikiza kanuni na mbinu fulani zenye lengo la kufanikisha uelewa wa lengo la Biblia na mitindo iliyotumiwa na wandishi wa MC kwa hadhira zao ambayo pia inawasilisha ujumbe wa MC kwa wasomaji wa leo.

3.3.1 Uhakiki wa Kihistoria

Uhakiki wa kihistoria kwa mujibu wa Obeng (1997) hulenga kuchunguza miktadha ya kihistoria ambamo matini fulani iliandikwa ili kubaini tukio lililofanyika au kuondoa utata kuhusu maana ya matini yenyewe. Mhakiki wa kihistoria hujishughulisha na kuweka mipaka kati ya mapokeo na ukweli wa kihistoria. Mathalan, kisa cha mwanamke Msamaria (Yoh. 4:1-45) huweza kueleweka vizuri katika muktadha wa mahusiano kati ya Wayahudi na Wasamaria hususan mwanamke kahaba. Mwanamke Myahudi alijitenga kabisa na mwanamke Msamaria na wala hawangeweza kukinywea kikombe kimoja naye. Yesu alithamini umuhimu wa binadamu na akapuuza mipaka hii ya kitabaka na kikabila kwa kusema naye na hata kumwomba maji ya kunywa. Hali kadhalika kwenda kwa Yesu karibu na Kisima cha Yakobo wakati wa mtikati (saa sita) kuna umuhimu wa kihistoria kwa hadhira ya MC na ML. Huu ndio wakati wenye joto jingi na hivyo tunaelewa kuwa alikuwa mchovu na mwenye kiu baada ya safari ndefu ya kutoka Uyahudi hadi mji wa Samaria uitwao Sikari.

3.3.2 Uhakiki wa Kimatini

Matini za kibiblia zimeathiriwa kwa kubadilishwa kimakusudi na kwa makosa ya kibinadamu katika mchakato wa karne kadha wa kuzipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano, mwandishi mchovu anaweza akafanya makosa bila kukusudia. Matini zinaweza pia kubadilishwa kimakusudi na wafasiri kwa nia ya kuzifanya kuwa na uhusiano na wakati wao au

kwa kukisia kwao kuzifanya kuwa bora zaidi. Hali kadhalika matini ziliweza kuathiriwa na ukuukuu au matumizi mabaya au ajali.

Lengo la uhakiki wa kimatini ni kurejelea kwa kadri iwezekanavyo kile ambacho waandishi wa Biblia waliandika katika miswada yao asilia. Mfasiri huanza kwa kuhakiki miswada iliyohifadhiwa kisha akarejea nyuma hadi kwenye miswada asilia. Kwa mantiki hii mfasiri ana nafasi bora anapokuwa na uelewa wa Kiebrania, Kiaramai na Kiyunani, ambazo ndizo LC. Kwa mfano, katika Luka 14:5 miswada asilia ya Kiyunani inabaini kuwa neno la Kiyunani ‘onos’ (punda) limeingizwa mahali pa neno ‘uios’ (mwana). Ingawa ujumbe unaosisitizwa na Yesu hapa ni kuwa maisha ya binadamu ni muhimu kuliko ya mnyama, kuwepo kwa tafsiri hizi mbili (‘ass’ katika KJV na ‘son’ katika NIV) kunaweza kukabainishwa tu kwa mfasiri kuwa na uelewa wa Kiyunani cha AJ. Kwa mujibu wa Odeng (1997) idhibati kutoka kwenye miswada bora zaidi inaonyesha kuwa mnakilishaji mmoja wa zamani alidondosha kimakosa neno ‘son’ na kuingiza neno ‘ass’ mahali pake.

Uhakiki wa kimatini ni mbinu inayohusu kulinganisha na kulinganua matini tafsiri ili kubaini tofauti zake. Tofauti hizi huangaziwa kwa misingi ya matini asilia kisha kubaini badiliko lililoingizwa ama kimakusudi au kwa kutokusudia. Kinachomwongoza mfasiri ni ubora na kiwango cha idhibati kutoka kwenye mswada, muktadha lugha na mtindo.

3.3.3 Uhakiki wa Chanzo

Uhakiki wa chanzo ni stadi ya matini za Biblia kwa lengo la kubaini chimbuko la habari za waandishi-ama kutoka kwa mazungumzo au vyanzo vilivyoandikwa. Baadhi ya vyanzo huelezwa wazi na waandishi (Taz. Luka 1:1-4). Vyanzo vingine havibainiki wazi isipokuwa kwa kuchunguza mabadiliko yasiyotarajiwa ya mtindo na msamiati, tofauti za kiusuli kati ya sura moja na nyingine inayoifuata, mabadiliko yasiyotarajiwa ya kimuundo kabla ya muundo wa awali kurejelewa upya, kuwepo kwa kisa kimoja mara mbili lakini kwa miundo tofauti na ukinzani wa kithiolojia unaodhaniwa kuwepo katika matini moja.

Vipengele muhimu vya uhakiki wa chanzo katika utafiti wa kibiblia ni matini ya kimasimulizi ya *Pentateuch* na *Synoptic Gospels (SG)*. *Pentateuch* imeelezwa kama matokeo ya vyanzo vinne-

Yahwist (j), Priestly (p) na Deuteronomist. Aidha chanzo cha SG kimekitwa katika hapothesia ya Marko na Q.

3.3.3.1 Chanzo cha Yahwist

Yahwist ni istilahi inayomrejelea mwandishi wa matini za AK zinazomtaja Mungu kama *Yahweh* ambazo zinaaminika ziliandikwa katika ufalme wa zamani wa Waisraeli ujulikanao kama Yuda wakati wa wafalme Daudi na Suleimani (950BC) . Mifano ya matini hizi ni kama vile Mwanzo 2-11, 12-16, 18-22, 24-34, 38 na 49; Kutoka 1-24., 32 na 34; Hesabu 11-12, 14 na 20-25; Waamuzi.

Hali kadhalika matini hizi zinahusishwa na matumizi ya neno *Yahweh* pamoja na majina fulani. Mathalan katika chanzo cha *Yahwist* jina la mkwewe nabii Musa ni Reul, mlima ule maarufu hutajwa kama Sinai na Wapalestina wanaitwa Wakanani, Kinyume cha chanzo cha *Elohist* ambamo mkwewe Musa ni Jethro, mlima ule unatajwa kama Horeb na Wapalestina wanaitwa Waamori (Amorites). Aidha kuna tofauti kuhusiana na kisa cha uumbaji ambapo *Yahwist* (Mwanzo 2:5-25) na *Elohist* (Mwanzo 1) vinatofautiana (<https://www.britannica.com/topic/Yahwist-source>).

3.3.3.2 Chanzo cha Elohist

Hiki ni chanzo cha matini zinazomtaja Mungu kama *Elohim*. Baadhi ya sifa bainifu za kimitindo za chanzo hiki ni urudiaji, mathalan “Ibrahimu, Ibrahimu” (Mwanzo 22) na “Musa, Musa” (Kutoka 3) na kutoangazia masimulizi ya kiukoo na uumbaji. Hapa tunatoa mifano ya matini za Ki-Elohist katika jedwali linalofuata:

Visa Muhimu vya Chanzo cha Elohist

ANWANI YA KISA	MAELEZO	MAREJELEO
Kisa cha Kiukoo	Ibrahimu kumtambulisha Sara kama Dadake	Mwanzo 20:1-18
	Ibrahimu kumtoa Isaka kama Kafara	Mwanzo 22:1-10, 16B-19
	Yakobo kushindana na Mungu	Mwanzo 32:22-32

	Kisa kifupi cha Yusufu	Mwanzo 37-50 (Pamoja na J na P)
Safari ya Kutoka Misri kwenda Kanani	Wakunga kuviua vitoto vya Kiebrania	kutoka 1:15-21
	Kijiti kuwaka moto bila kuteketea	Kutoka 3:1-15 (Pamoja na J)
	Safari ya Kutoka Misri	Kutoka 13
	Visa vya Jangwani	Kutoka 17-18
	Kuonekana kwa uwepo wa Mungu (Theophany)	Kutoka 19:1-9
	Amri Kumi	Kutoka 20:1-17 (Pamoja na P)
	Kitabu cha Agano	Kutoka 20:18-23:33
	Sherehe ya Agano	Kutoka 24:1-18 (Pamoja na P)
	Ibada ya Sanamu ya Ndama iliyotengenezwa kwa dhahabu	Kutoka 32-33
Kadhia za Jangwani	Manung'uniko na Migogoro	Hesabu 11-12
	Nabii Balamu wa Wamoabu	Hesabu 22-24

Chanzo: barrybandstra.com/tables/pt1-tb3

3.3.3.3 Chanzo cha Ki-Priest

Wasomi wa Biblia wanahoji kuwa Chanzo cha Ukuhani ndicho chimbuko la sherehe na sheria za ibada na utoaji kafara hususan baada ukuhani kuanzishwa na Mungu katika jangwa la Sinai. Halikadhalika chanzo hiki kinahusishwa na hadhi ya juu ya ukuhani na matumizi ya istilahi *El Shadai* kabla ya Mungu kujifunua kwa Musa. Chanzo cha 'P' kinasisitiza utakatifu wa taifa la Israeli kwa kuzingatia sheria na sherehe za kafara na kutooana na watu wa mataifa mengine. Baadhi ya mifano ya chanzo cha P ni Kutoka 25-31 na 35-40; Mambo ya Walawi 1-26 na Hesabu 1-10: 28, 15-20, 25-31 na 33-36. ([https://www.revolvy.com/topic/priestly source & item-type=topic](https://www.revolvy.com/topic/priestly+source+&+item-type=topic)).

3.3.3.4 Chanzo Ki-Deuteronomy

Chanzo cha *Ki-Deuteronomy* hutumia msamiati na mtindo bainifu kuwahimiza Waisraeli wazingatie sheria za Agano la Yahweh na kuisitiza uteuzi wake wa Israeli kama taifa teule.

Chanzo hiki kinahusishwa na vitabu vya Kumbukumbu la Torati, Yoshua, Wamuzi, Samueli, Wafalme na baadhi ya manabii (mathalan, Yeremia). Matini hizi zilitumika kufundisha makubaliano na zilitumia lugha, dhana na mitazamo ya kithiolojia inayoshahibiana na kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Chanzo hiki kiliangazia uaminifu na utiifu kwa Mungu kama njia mwafaka ya kumtukuza Mungu kwa neema yake. Aidha chanzo hiki kilijumwisha matini za kisheria zijulikanazo kama Torah.

3.3.3.5 Chanzo cha Marko na Q

Kwa mujibu wa haipotesia ya vyanzo viwili vya SG kitabu cha Marko ndicho kilichokuwa cha kwanza kutungwa na hivyo waandishi wa Mathayo na Luka walikitumia pamoja na matini ijulikanayo kama *Chanzo cha Q* walipokuwa wakiandika injili zao. Ijapokuwa mapokeo ya kale ya Kikristo yanadai kuwa matini hii iliandikwa na John Mark (mwandani na mkalimani wa mtume Petro) wasomi wengi wa Biblia wanahoji kuwa mwandishi wake hajulikani. Aidha wanadai kuwa mwandishi alitumia aina kadha za vyanzo vya awali (mathalan, masimulizi ya migogoro katika Marko 2:1-3:6, mjadala kuhusu matukio ya mwisho wa dunia katika 4:1-35 na mkusanyiko wa misemo). Yamkini mwandishi alishawishiwa na fasihi ya Wayunani na Warumi (Greco- Roman Literature) na alichota marejeleo yake yote kutoka katika maandiko ya Wayahudi katika tafsiri ya LXX.

Kietimolojia chanzo cha Q kimetokana na herufi ya kwanza ya neno la Kijerumani, yaani *quelle*, kwa maana ya chanzo. Kwa mujibu wa haipotesia hii, chanzo cha Q hakijulikani isipokuwa kwa Mathayo na Luka ambao ndio waandishi wa vitabu vya Mathayo na Luka. Hali kadhalika uhakiki huu unahoji kuwa wasomi wa Biblia hawakubaliani iwapo ama chanzo cha Q ni maandishi au ni masimulizi ya kimapokeo ambayo waandishi hawa wawili waliyashiriki. Hata hivyo kwa kuhakiki data katika matini hizi, kila moja ikitengwa na nyingine, HL ya mwandishi inabainika wazi. Mathalan, Mathayo ina unukuzi zaidi wa AK kuliko vitabu vingine vya injili. Hivyo HL ya Mathayo ilikuwa Wayahudi ili kuwathibitishia kuwa Masihi aliyesubiriwa kwa muda mrefu alitimiza unabii wa AK. (<https://en.m.wikipedia.org>)

3.3.4 Uhakiki wa Umbo

Uhakiki wa Umbo umekitwa katika jamii ambamo masimulizi yalichipuka ili kubainisha umbo na uamili wake kabla hayajaandikwa. Hoja muhimu hapa ni kuwa kila jamii ilihitaji kutumia aina fulani za misemo katika fasihi simulizi, mathalan; visasili, nyimbo, methali na shukrani. Kila kimojawapo cha aina hizi za mitindo kilitumikizwa katika muktadha maalum wa jamii.

Umbo humwezesha uhakiki kupata uelewa wa utamaduni wa jamii husika na matatizo yaliyoikabili. Uhakiki wa umbo umekitwa katika kanuni nne:

- (i) Matini za *Synoptic Gospels* (*Mathayo, Marko na Luka*) ni fasihi pendwa wala si tungo zinazotumia lugha kisanaa. Kwa mantiki hii wasomi wa Biblia wanahoji kuwa wainjilisti hawakuwa wanahistoria waliotumikiza mbinu za kisasa za utafiti bali walikuwa wahawilishaji wa mapokeo muhimu ya Wakristo.
- (ii) Kulikuwa na kipindi kati ya huduma ya Yesu na uandishi wa matini za Injili ambamo maneno ya Yesu yaliwasilishwa kimasimulizi.
- (iii) Maneno haya pamoja na masimulizi kumhusu Yesu yalienea kama vipashio huru katika kipindi hiki cha masimulizi na yamkini yalikusanywa pamoja kabla ya kuandikwa kwa injili ya kwanza.
- (iv) Katika kipindi cha masimulizi, vipashio hivi vya kimapokeo vilichukua umbo maalum kulingana na uamilifu wake katika jamii ya Wakristo. Wahakiki wa umbo wanahoji kuwa kuna aina tano za maumbo ya injili; violezofaridi (*paradigms*), hadithijasira (*tales*) visakale (*legends*), visasili (*myths*) na mahimizo (*exhortations*).

3.3.5 Uhakiki wa Ki- Historia Mapokeo

Uhakiki wa Ki-historia Mapokeo umekitwa katika nyenzo za kihistoria ama za kimasimulizi au zilizoandikwa na hulenga kuonyesha jinsi nyenzo hizi hubadilika kwa misingi ya umbo. Hivyo huu ni uhakiki ambao umepata mihimili yake kutokana na Uhakiki wa Umbo. Mbinu hii ya uhakiki huwa sahili zaidi pale ambapo ujumbe fulani unatokeza mara mbili kwa maumbo mawili tofauti; hivyo, ama mmoja huonekana kupata ubora wake kutokana na ule mwingine au yamkini maumbo yote mawili yalitokana na umbo asilia moja, yakiwa yamekuzwa katika sehemu na mazingira tofauti.

Baadhi ya mifano ya ujumbe unaotokeza mara mbili kwa maumbo tofauti katika AK ni ule wa Amri Kumi katika Kutoka 20:2-17 na Kumbukumbu la Torati 5:6-21. Orodha ile ile ya amri inatokeza mara mbili lakini zikitofautiana kwa kuwa kila mojawapo ina kiarifu tofauti. Katika AJ mfano mwafaka ni pale ambapo Petro anatoa majibu tofauti kuhusu swali moja lililoulizwa na Yesu kuhusu kitambulisho chake katika mji wa Kaisari Filipi. Injili zote tatu zinataja kuwa kadhia hii ilifanyika katika mji wa Kaisari Filipi lakini kila matini inawasilisha majibu tofauti. (Taz.Mk. 8:29; Mat.16:16; Luk.9:20). Mhakiki ana jukumu la kubaini ni jibu lipi asilia na ni vipi majibu yale mengine yaliibuliwa? Aidha ufufuo wa Yesu una masimulizi mawili tofauti: tafsiri ya Marko (16:1-18) kuwa Mariamu alifika na wanawake wenzake na wakampata mwanaume aiyevalia vazi jeupe(malaika) ambaye aliwatangazia habari kuwa Yesu alifufuka; katika Yohana 20:1-8 Mariamu anawasili peke yake kisha anakimbia kuwaita Petro na mwanafunzi mwengine, malaika wawili wanawatokea bila kuwaambia kuwa amefufuka lakini wanakutana na Yesu mwenyewe. Tofauti kama hizi huelezwa kwa misingi ya uhakiki na Ki-historia Mapokeo.

3.3.6 Uhakiki Hariri

Uhakiki Hariri huangazia kazi ya uhariri iliyofanywa na waandishi wa Biblia kwa vyanzo vyao-yaani, ni stadi ya mabadiliko bainifu yaliyoingizwa na waandishi katika vyanzo vya kimapokeo walivyovipokea. Aidha huu ni uhakiki unaojishughulisha na utambuzi wa michango ya kisanaa ya waandishi kwa mapokeo ya Kikristo wanayoihawilisha. Matini za *Synoptic Gospels* ni mfano mwafaka wa kazi zinazoweza kuhakikiwa kwa mbinu hii kuwa kuwa kwa muhibu wa Obeng (1997) tofauti kati matini hizi zilitokana na juhudi za kimakusudi za waandishi za kufinyanga vyanzo vyao ili kutimiza malengo yao maalum.

Shughuli muhimu katika zoezi hili la uhakiki ni pamoja na kuchunguza kwa umakinifu jinsi ambavyo vyanzo viliunganishwa, mikhtasari, uvumishaji, uchopekaji na udodosaji uliofanywa, kwa jumla uteuzi na upangaji wa vyanzo. Hali kadhalika mhakiki anashurutika kuchunguza msamiati wa mwandishi, mtazamo wake wa kithiolojia na jinsi anavyotanguliza na kuhitimisha Injili yake. Mathalan, mwandishi wa Mathayo anaaminika aliandika Injili yake kwa kuhariri vyanzo vya Mark, Q na M (chanzo maalum cha Injili ya Mathayo ambacho si ‘Mark’ wala ‘Q’). Ameingiza uelewa wake wa ufasiri wa mapokeo ya Kikristo kumhusu Yesu kwa kuteua na

kupanga vyanzo vyake kwa namna ambavyo inamchora Yesu kama Mfalme na Mtumishi asiye puuza sheria wala Injili. (Taz.Edwards, 2009).

Kabla ya kuhitimisha tathmini ya mbinu za uhakiki wa matini za Biblia ni muhimu kutaja hapa kuwa mbinu za uhakiki zilizojadiliwa si huru bali zinachangizana na kila moja huchota kutoka kwa nyingine katika kutumkizwa kwake. Mhakiki wa umbo anahitaji uelewa wa uhakiki wa chanzo ili kubaini historia ya kiufasihi ya mapokeo, kwa kadiri iwezekanavyo, kabla ya kutoa hoja kuhusu kipindi cha masimulizi; vivyo hivyo mhakiki hariri anaweza kutoa maoni ya kutegemewa kuhusu mitindo ya uhariri ya mwandishi ikiwa tu ataelewa vyanzo vilivyotumiwa na mwandishi. Aidha kuna ugiligili kati ya uhakiki wa ki -historia mapokeo na uhakiki hariri kwa kuwa maoni ya mhariri hutambulisha hali yake katika kundi la mitume na matatizo ambayo yeye na jamii yake walikumbana nayo. Hali kadhalika uhakiki hariri hukitwa katika uhakiki wa umbo kwa kuwa umbo huwezesha kubainika kwa kazi za kila mwandishi.

3.4 Aina za Matini za Tafsiri

Aina za matini (text typology) ni istilahi inayorejelea msingi wa kidhana unaotuwezesha kuainisha matini kwa kigezo cha malengo ya kimawasiliano yenye jukumu la ushawishi wa lugha (*rhetorical purpose*). Hivyo kwa kutathmini uamili wa kimawasiliano mbali na aina ya matini tunaweza kueleza nduni za matini za tafsiri. Baadhi ya aina za matini ni kama vile masimulizi, maelezo (descriptive), fasili (*expository*) mjadala (*argumentative*) na uhusika (*instrumental*). Kwa mujibu wa Hatim na Mason (1990) uanishaji wa matini umekitwa katika taratibu za kimawasiliano, pragmatiki na semiotiksi (*semiotics*) zinazozingatiwa wakati matini inaingizwa katika muktadha wake. Taratibu hizi ni za kijumla (*macro-text processing*) na zile zisizo za kijumla (*micro-text processing*) na hutumikizwa kwa pamoja katika kubaini ni jinsi gani aina ya matini inashawishi maamuzi ya mfasiri. Mchakato wa ‘*micro*’ unahusu uamilifu wa kimawasiliano na aina ya matini na kiwango cha ‘*macro*’ huangazia tendo la matini. (Tazama Trosborg 2002, Reiss 2004).

Aidha istilahi nyingine zinazotumika kurejelea aina za matini ni diskosi (usemi), sajili na utanzu (genre). Katika utafiti wetu tumetumia istilahi hii kwa maana ya aina za kaida (norms) za matini zinazotumiwa katika miktadha maalum ya mawasiliano. Uelewa wa miundo ya matini na kaida

zinazozibainisha hufanikisha upatikanaji wa tafsiri bora. Hata hivyo tumeeleza kuwa matini nyingi si za kaida moja tu bali huwa ni mchanganyiko wa miundo tofauti (mathalan, Ayubu ni mchanganyiko wa shairi na dayalojia).

3.4.1 Matini ya Kimjadala

Matini ya kimjadala ni matini inayotumiwa ama kutetea au kupinga imani, dhana au kauli fulani. Baadhi ya nduni, zake ni kama vile kuakisi sababu, umuhimu, kauli, thamani na upinzani wa misimamo fulani. Aidha matini hii huonyesha mshikamano katika vipengele vinavyosisitiza hoja yake (mathalan urudiaji, usambamba na ufafanuzi). Mwandishi wa matini ya kimjadala hutetea hoja zake kwa namna ambavyo malengo yake yanafaidi (*situation managing*). Aidha anwani ya matini ya kimjadala huwa ndicho kiunzi cha mjadala wenyewe hivyo mwandishi anashurutika kuiweka bayana. Kwa jumla nduni muhimu za matini ya Kimjadala ni mtazamo wa kulinganisha, kuhoji na kuthamini, unukuzi wa watu, matumizi ya vitenzi kisemantiki (mathlan kuona, kuhisi, kusema n.k), wingi wa matumizi ya miundo fulani ya kisintaksi (mathalan kauli tendwa na uelekezi), matumizi ya mada nzito zenye ukwasi wa istilahi n.k.

3.4.2 Matini Fasili

Matini fasili huangazia uchanganuzi wa elementi za dhana fulani au muungo (composition) unaotokana na elementi zake. Mwandishi wa matini fasili hulenga kutoa maelezo yenye mantiki kuhusu hali fulani pasi na nia ya kudhibiti hali yenyewe (*monitoring of the situation*). Katika fasili mada ya matini haibaniki wazi pale mwanzo, hivyo mwandishi hutumia maelezo kamili kuhusu mada yenyewe anapotoa hoja zake hatua kwa hatua. Miundo ya kisintaksia na kisemantiki ya matini fasili huwa sahili ikilinganishwa na ile ya matini ya kimjadala.

3.4.3 Matini Elekezi

Nduni muhimu ya matini elekezi ni kishawishi tabia za wasomaji kwa kuwafunza jinsi wanastahili kutenda na kifikiri. Kuna aina mbili za matini elekezi: zile zinazompa msomaji nafasi ya kuchagua atakalo (mathalan matangazo ya biashara, ushauri kwa wateja n.k) na zile zisizotoa nafasi ya kuchagua kwa msomaji (mathalan mikataba na maazimio rasmi). Katika Biblia mfano wa matini elekezi ni Kutoka 20 (amri kumi za Mugu). Ili kufanikiwa katika

kuwashawishi wasomaji kutenda na kufikiri kama ilivyokusudiwa sharti matini elekezi iwe na sifa kadha muhimu:

3.4.3.1 Usahili

Usahili unahusu matumizi ya sentensi fupi fupi, sintaksia na istilahi sahili zisizoibua utata kwa wasomaji. Mwandishi hana budi kutumia msamiati sahili ili wasomaji wasitumie nguvu nyingi kuelewa ujumbe wa matini yake. Matumizi ya mbinu za kisanaa kama vile homonimi, misemo, nahau na jazanda, sitiari na tabaini yafanywe kwa umakinifu.

3.4.3.2 Utopiki

Matini sharti iakisi uhalisia wa maisha kwa kutumia maneno faafu, mada zinazoshawishi n.k. Mwandishi anashurutika kutoa taswira halisi ya maisha ya kikawaida. Hivyo topiki ya matini elekezi hukitwa katika mazingira halisi ya jamii na kujaribu kuyasawiri kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi.

3.4.3.3 Ukumbukwaji

Matini elekezi sharti itumie mbinu zinazowawezesha wasomaji kukumbuka ujumbe wake bila ugumu wowote. Mbinu hizi ni kama vile urudiaji, matumizi ya msamiati teule, wizani, muwala, usambamba, mpangilio wenye mantiki wa mawazo na mfuatano wenye mantiki wa hoja zinazotolewa.

3.4.3.4 Uvutiaji

Hii ni mbinu ya kushawishi kauli za wasomaji kwa kusisitiza, kuonyesha faida ya maamuzi fulani, kudokeza n.k. Matangazo ya kibiashara hukuza sifa hii kwa kutia chumvi katika habari zake. Hoja muhimu hapa ni kuwa kwa kadiri iwezekanavyo matini elekezi huegemea kwa hadhira yake.

3.4.3.5 Utekenyaji Hisia

Huu ni uwezo wa matini kuzitekenya hisia za hadhira kwa mguzo wa kipekee ili iathirike upesi na kwa urahisi. Hadhira ipate hasira, furaha, huzuni, hofu au huruma kwa mvuto wa nguvu. Nduni hii ni muhimu kwa kuwa huwezesha muamala kati ya mwandishi na hadhira yake.

3.4.3.6 Unyumbuaaji wa Lugha

Mwandishi yuko huru kufinyanga lugha kwa namna ambavyo propaganda inawasilishwa kama habari kupitia kwa mbinu kama vile usambamba wa kiisimu (ili kuonyesha ukweli na ukubalifu) na ufananishi. Kwa mantiki hii, mwandishi anatumia lugha kutagusana na hadhira.

3.4.3.7 Kuaminika

Huu ni uwezo wa matini kuwashawishi wasomaji hata kama ujumbe wake ni mchanganyiko wa kweli na uongo. Mwandishi hulenga kuwashawishi wenye mamlaka, mashahidi “wataalam” naumma kwa lugha yenye mnato na kwa namna ambavyo si rahisi kwa hadhira kutokuwa na imani na matini yake.

3.4.4 Masimulizi

Masimulizi ni kisa cha matukio ama ya kweli au ubunilizi, ambacho mwandishi amekipa umuhimu fulani. Masimulizi ya kweli ni kama vile ripoti za magazeti, maungamo na rekodi za kihistoria; aidha ubunilizi ni kama vile, futuhi ya kujiambua (*comic strips*), tenzi, nyimbopendwa (ballads), novela na hadithi fupi za kiubunilizi. Masimulizi huwa na msuko, fomula funguzi na fungizi, ama kilele au mpomoko. Aidha nduni nyingine ya masimulizi ni matumizi njeo iliyopita. Baadhi ya mifano ya masimulizi katika Biblia ni Mwanzo 1 (kisa cha uumbaji), Luka 1:5-80; 3:1-22 (kisa cha Zakaria na Yohana) na Matendo ya Mitume 2 (siku ya Pentekote). Ufuatao ni upambanuzi wa aina za masimulizi kwa mujibu wa Baker (2006):

3.4.4.1 Masimulizi ya Kisayansi

Istilahi hii hurejelea masimulizi ambayo huhalalisha kategoria za tabia, matukio na hususan kwa malengo ya kisiasa. Mathalan, mtazamo wa kisayansi katika karne ya kumi na sita kuhusu tofauti kati ya weusi na weupe uliohoji kuwa watu wote walizaliwa sawa lakini mazingira ambamo tunazaliwa huikilia nafasi yetu katika rangi za mataifa ya ulimwengu- weupe huchukua nafasi ya kwanza na weusi nafasi ya mwisho. Hivyo mtu mweusi angeweza kuwekwa katika kiwango sawa na mtu mweupe kutoka bara Uropa ikiwa anghamishwa kutoka bara Afrika na kupelekwa katika mazingira ya watu weupe akiwa mchanga. Masimulizi haya yalitumiwa kuhalalisha biashara ya utumwa na ubaguzi wa rangi hususan nchini Afrika Kusini. Kutokana na mfano huu

ni bayana kuwa masimulizi ya kisayansi huwa na lengo la kuhalalisha vitendo na misimamo fulani katika ulimwengu halisi.

3.4.4.2 Masimulizi ya Umma

Masimulizi ya Umma kwa mujibu wa Ganz (2008) ni mchakato huru (*discursive process*) unaowezesha watu binafsi, jamii, na mataifa, kufanya maamuzi, kujitambulisha na kuchochea vitendo. Aina hii ya masimulizi hushawishi nia, huelekeza jinsi ya kutenda na kumhimiza msomaji kuchukua hatua fulani. Masimulizi ya umma yana elementi tatu muhimu: mtu binafsi, jamii na uamuzi. Kisa cha mtu binafsi hurejelea maadili, maamuzina tajiriba yake. Elementi ya jamii hurejelea maadili, tajriba na maamuzi ya jamii na elementi ya uamuzi hurejelea wakati wa changamoto, matumaini na uchaguzi. Hivyo masimulizi ya umma huchochea vitendo katika tamaduni, dini, taaluma, matabaka na nyakati mbali mbali.

Ganz anahoji kuwa masimulizi ya umma si uzungumzi wa umma (*public speaking*) bali ni sanaa ya uongozi inayomwezesha msomaji kutenda kulingana na maadili. Ploti, uhusika, maudhui na mandhari ya masimulizi ya umma vina uamilifu muhimu. Ploti huwasilisha changamoto, uchaguzi na matokeo yake, hivyo huwezesha kukabaliana na yale yasiyotarajiwa; uhusika husisitiza kitambulisho kupitia kwa nguli, maudhui hufunza maadili na mandhari hujenga mahusiano kwa kuhimiza mtagusano wa kimaadili. Mfano wa masimulizi ya umma katika Biblia ni mjadala kati ya Musa na Mungu ambapo Musa anauliza maswali (Kwa nini mimi? Nani anayenituma? Kwa nini Waisraeli na Wamisri? Kwa nini sasa na hapa?) wakati Mungu anapomwita ili awakumboe Waisraeli kutoka utumwani. Musa anadadisi tajiriba yake, Mungu, Wamisri na Waisraeli na kwa mantiki hiyo kuamua kukabiliana na Farao na Safari ngumu ya kutoka Misri kwenda Kanani.

3.4.4.3 Masimulizi ya Kiontolojia

Simulizi la kiontolojia hujishughulisha na asili ya uhai na maisha. Mathalan, mjadala wa kiontolojia kumhusu Mungu hutoa hoja kadha: Mungu ni mkuu kuliko vyote na anaishi si katika mawazo tu bali pia katika uhalisi wa hali; Mungu ni mkamilifu na ukamilifu wake ndio unaomfanya kuwa Mungu. Kiini cha uhai ni Mungu; Mungu na uhai havitenganishiki; Mungu ni Uhai na Uhai ni Mungu. Haiwezekani kuwa mwanadamu alijiumba (panahitajika uhalisi, uwezo

na ukamilifu kuumba kitu, mathalan, sifa za kiasili na ubora). Kwa mantiki hii ikiwa mwanadamu amejiumba, basi angekuwa na uwezo wa kujiambia tabia kamilifu (ambao hakuna kisichodumu milele kinacho). Mwanadamu hajakuwepo milele wala hana uwezo wa kudumisha uhai hata kwa kitambo kidogo, mtu hawezi akadai kuwa alitokana na wazazi wake (ambao walitokana na wazazi wao n.k). Hivyo mwanadamu hana budi kuchukulia kuwa Mungu mkamilifu na mwenye uwezo usio kifani yupo, na ndiye chimbuko la uhai wake na kwa mantiki hii kuiweka dhana ya Mungu mawazoni mwake.

Aidha aina nyingine ya masimulizi ya kiontolojia ni visa ambavyo watu hutoa kuhusu maisha yao. Masimulizi hayo hushawishi nafasi ya watu katika jamii na matendo yao. Aghalabu anayesimulia huwa ndiye nguli. Chimbuko la simulizi la kiontolojia ni ule upekee wa historia ya mtu binafsi. Mifano ya aina hii ya masimulizi ni kama vile tawasifu ya mtu aliyenusurika kifo wakati wa mauaji ya halaki, ushahidi wa mwathiriwa wa unajisi mahakamani na simulizi kuhusu tajriba ya utotoni.

3.4.4.4 Masimulizi Dhanifu

Masimulizi dhanifu ni dhana na maelezo ambayo hubuniwa na watafiti; ni masimulizi yanayohusiana na taaluma fulani ya kiusomi. Kwa mujibu wa Baker, haya ni masimulizi ambayo wasomi katika taaluma yoyote hutumia kujieleza kuhusiana na malengo yao ya utafiti. Aina hii ya masimulizi pia huwa na mwanzo, kati na mwisho. Dhima ya masimulizi dhanifu na kutusaidia kupata maana ya ulimwengu wetu; yaani eneo letu la utafiti. Mifano ya masimulizi dhanifu ni kama vile nadharia ya Darwin ya mchujo wa kiasili (*natural selection*) na simulizi la migogoro ya waliostaarabika (*Clash of Civilizations*) ambalo limeibua masimulizi ya Vita Dhidi ya Ugaidi katika siku za hivi karibuni (<https://artisinitiative.org/online-course-2>).

3.4.4.5 Masimulizi ya Kimataifa

Masimulizi ya kimataifa ni masimulizi yaliyo na ushawishi mkubwa kimataifa. Masimulizi ya umma na masimulizi dhanifu yaliyokuzwa na kutumikizwa katika matukio mengi tofauti hatimaye hugusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni na kufanyika kuwa masimulizi ya kimataifa na kwa mantiki hii, masimulizi ya kimataifa hupita mipaka ya kitamaduni na kimaeneo na huwa na ushawishi mkubwa katika siasa za kimataifa. Kwa mujibu wa Baker taaluma ya

tafsiri hutekeleza jukumu muhimu la kukuza masimulizi ya umma na masimulizi dhanifu hadi kufikia kiwango cha masimulizi ya kimataifa. Baadhi ya mifano ya masimulizi ya kimataifa ni kama vile 'Progress' 'Decadence,' 'Enlightment', Ubepari dhidi ya Ukomunisti (Capitalism vs Communism) 'Class struggle,' Mauaji ya Halaiki (Holocaust) na Vita dhidi ya Ugaidi (War on Terror).

3.4.5 Mashairi

Shairi ni aina ya matini yenye ukuishi mwingi kuliko aina nyingine za matini. Baadhi ya nduni za shairi ni matumizi ya jazanda kwa wingi, ukiushi wa kimofolojia na kisintaksia (mathalan tabdila na mpangiolo pindu wa maneno), uchimuzi, urudiaji na usambamba. Hali kadhalika shairi hubainishwa kwa arudhi; wizani, lugha mkato, muwala, mizani, mishororo na ubeti. Shairi huru halizingatii arudhi kwa kuwa mwandishi hutumia uhuru wa ushairi kujieleza atakavyo. Baadhi ya mashairi katika Biblia ni kama vile Isaiah 53, Zaburi, Mhubiri, Ayubu, Methali na Wimbo ulio Bora.

Wataalam mbalimbali wa ushairi wameanisha mashairi kwa kuzingatia vigezo vitano vikuu, yaani idadi ya mishororo katika kila ubeti, urari wa mizani, mtiririko wa vina, idadi ya vipande vya mishororo na mpangilio wa maneno katika mishororo na ubeti. Kigezo cha idadi ya mishororo huzalisha bahari kama vile tathmina, tathnia, tathlitha, tarbia, takhmisa na tasdisa; urari wa mizani unabainisha bahari kama vile kikai na msuko; mtiririko wa vina huzalisha aina za mtiririko, ukara wa ukaraguni; idadi ya upande vya mishororo inabainisha bahari za mathnawi, ukawafi na mavue. Aidha mpangilio wa maneno katika mishororo au ubeti huzalisha mkufu, kikwamba na mandhuma.

Bahari nyingine za mashairi ni ngonjera, sibilila na mashairi picha. Hali kadhalika yapo mashairi huru na mashairi jadi (Arege 2013). Mashairi mengi katika Biblia yanaweza kuaninishwa kama mashairi huru kwa kuwa hayazingatii urari wa vina na mizani wala hayana vibwagizo. Shairi lifuatalo linawakilisha muundo wa mashairi ya kibiblia:

1.Haleluya.

Msifuni Mungu katika

patakatifu pake;

Msifuni katika anga la uweza

wake.

2.Msifuni kwa matendo yake

makuu;

Msifuni kwa kadiri ya wingi

wa ukuu wake.

3.Msifuni kwa mvumo wa

baragumu;

Msifuni kwa kinanda na

kinubi;

4.Msifuni kwa matari na kucheza;

Msifuni kwa zeze na filimbi;

5.Msifuni kwa matoazi yaliayo;

Msifuni kwa matoazi
yavumayo sana.

6.Kila mwenye punzi na amsifu

BWANA.

Haleluya.

(Zaburi 150, SUV)

3.4.6 Dayalojia

Matini ya kidayalojia imekitwa katika mtagusano wa kimazungumzo, unaohusu kubadishana mawazo au mtindo wa maswali na majibu kati ya wahusika wawili au zaidi. Aidha dayalojia huingizwa katika masimulizi kupitia kwa usemi wa wahusika kama vile katika drama. Tamthilia na mashairi ya kidrama ni aina za dayalojia ambazo zimekusudiwa kuigizwa kwa mazungumzo na vitendo vya ploti. Katika dayalojia kila tamko au sentensi hutarajia jibu ili kufanikisha mtagusano kati ya wahusika. Baadhi ya mifano ya dayalojia katika Biblia ni Ayubu 4 - 14 (kati ya Ayubu na rafikize kuhusu mateso yake) na Mwanzo 18:23-33 (kati ya Mungu na Ibrahimu kuhusu kuangamizwa kwa miji ya Sodoma na Gomora). Hali kadhalika kuandikiana barua, kujaza fomu rasmi na hojaji ni dayalojia za aina yake. (Taz. Wales,2001)

3.4.7 Matini Fafanuzi

Matini Fafanuzi ni matini inayoeleza vile mtu au kitu kilivyoye. Jukumu lake ni kueleza na kubainisha mtu, pahali au kitu fulani. Muundo wa matini fafanuzi ni sahili: kwanza hubainisha kinachoelezwa kisha hukieleza kwa kuangazia sehemu zake, sifa au nduni. Hali kadhalika lugha ya matini ya fafanuzi husheheni vielezi, nomino za aina mbali mbali na matumizi ya njeo sahili wakati uliopo. Matini fafanuzi huweza kuainishwa pia kama aina ya matini arifu. Hapa tunanukuu mfano wa matini fafanuzi kuhusu hekalu lililotumiwa na Waisraeli katika jangwa la Sinai:

Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada,na patakatifu pake,pa dunia.Maana hema ilitengenezwa,ile ya kwanza,mlimokuwa na kinara cha taa,na meza,na mikate ya Wonyesho;ndipo palipoitwa ,Patakatifu.Na nyuma ya pazia ya pili,ile hema iitwayo Patakatifu pa patakatifu,yenye chetezo cha dhahabu,na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote,mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile maana,na ile fimbo ya Haruni iliyochipuka,na vile vibao vya agano;na juu yake makerubi ya utukufu,yakikitia kivuli kiti cha rehema;basi hatuna nafasi sasa ya kuvieleza vitu hivi kimoja kimoja. (Waebrania 9:1-5,SUV)

3.5 Muhtasari

Sura hii imewasilisha matini chanzi za Biblia, mbinu kadha za uhakiki wa matini hizo na aina za matini.Kama ilivyoelezwa awali vipengele hivi ni muhimu katika kumwezesha mfasiri hususan wa matini ya kibiblia kuteua mbinu atakayoitumia kutafsiri matini anayoishughulikia. Imedhihirika kuwa ubora wa kazi ya mfasiri unahusishwa kwa kiwango fulani na uelewa wa hoja zilizojadiliwa hapa. Tumehoji kuwa kuzitambua nduni za utanzu unaofasiriwa kuna natija

kwa mfasiri kwa kuwa ndizo huakisi uamilifu wa kimawasiliano wa MC. Aidha tumemaliza sura hii kwa kuhoji kuwa mjadala huu umetoa njia na mikakati faafu ya uchanganuzi wa data yetu ya upili kwa mitazamo ya Tafsiri Kimawasiliano na Tafsiri Kielimumitindo.

SURA YA NNE

NAFASI YA AINA ZA MATINI KATIKA KUSHAWISHI MBINU ZA TAFSIRI

4.0 Utangulizi

Tafakuri yetu kuhusu tafiti za awali katika stadi ya tafsiri ni kuwa ukiwa umejikita katika nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri kwa kuwa tafiti nyingi zimekitwa katika maswala kama vile ulinganifu na ufaafu wa maana katika kiwango cha maneno na sentensi, changamoto za kutafsiri kutoka LC hadi LL na usonde katika tafsiri. Kwa matiki hii tutafanya uchanganuzi wa aina za matini katika Mwanzo II, kutoka 20 na Zaburi 23 pamoja na nafasi ya aina hizi za matini katika kushawishi maamuzi ya mfasiri kuhusu mbinu faafu za kuzitafsiri. Katika kushughulikia suala hili tumeonyesha kuwa kila matini ina upekee wake wa umbo ambao mfasiri anashurutika kuuzingatia ili kufanikisha uhawilishaji wa ujumbe wa MC. Hii ina maana kwamba kwa kiwango fulani kila mfasiri ana jukumu la kustahabali (*specialize*) katika kuchunguza vipengele vya kiisimu vinavyotambulisha aina mbali mbali za matini. Uelewa wa aina ya matini inayotafsirirwa kwa mujibu wa Ruzaita (2006) pia unahusisha uelewa wa msingi wa kijamii na kitamaduni ya MC na ni jambo lisiloepukika kwa kuwa hurahisisha kazi ya mfasiri. Anahoji kuwa ulinganifu katika tafsiri si suala la maneno na sentensi tu bali pia kuna kiwango cha aina ya matini kwa kuwa aina tofauti za matini zina uamili tofauti wa kimawasiliano. Hali kadhalika tunasisitiza kuwa katika kubainisha aina ya matini lengo la matini yenyewe ni kigezo muhimu.

4.1 Uchanganuzi waTafsiri ya Zaburi 23

Yamkini Zaburi 23 ndiyo matini ya kishairi ambayo ni maarufu zaidi katika AK. Kama ilivyoelezwa, baadhi ya vipengele vinavyolipatia ushairi upekee ni mpangilio wa sauti wenye mapigo ya kimuziki na wizani, kusema mengi kwa maneno machache yenye kunata, matumizi bora ya picha, ishara na tamathali za semi na ukiukaji wa mfuatano wa kawaida wa maneno katika tungo. Nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano inasisitiza ML ihawilishe athari ya MC kwa HL, hivyo yafaa mfasiri afikirie umbo la MC ya kishairi kwa kuwa uwezo wa kuathiri linalokuwa nalo shairi unatokana na lile umbo lake maalum. Tunahoji kuwa fani na maudhui yake havitenganishiki na vyote vimekitwa katika lile umbo lake maalum. Tunadokeza hapa kuwa mfasiri wa Zaburi 23 afikirie na kuvitumia vipengele vya fani kwa makini na kwa kadri

iwezekunavyo kulihawilisha umbo lake ili kuhifadhi maudhui na umbuji wake wa kisanaa na kuzitekenya hisia za HL.

Jeffrey (2012) anahoji kuwa changamoto kubwa zaidi inayowakabili wafasiri wa kisasa wa matini ya kishairi katika Biblia ni mwelekeo hasi wa HL kuhusu lugha ya kishairi na mamlaka yake. Anadai kuwa wasomaji wengi wa tafsiri za kishairi hawana ushairi wala heshima kwa mamlaka ya uungu inayowasilishwa katika Maandiko Matakatifu kwa lugha ya ushairi. Hii ni kwa sababu wasomaji wengi huwa na chukulizi kuwa lugha shairi haina mashiko (*ephemeral*) na ina utata usiohitajika. Kwa mantiki hii yafaa mfasiri wa matini ya kishairi aepuke kutoa tafsiri tenge kwa kutumia lugha ya kinathari (iliyo ya kawaida na yenye maelezo) kwa kujaribu kutosheleza matarajio ya msamiati na mwanoulimwengu wa HL. Mfasiri wa matini yoyote ya Biblia hususan mashairi anahitajika kutambua kuwa matumizi ya lugha ya kitamathali na polisemia ni nduni muhimu ya MC ambayo haina budi ihawilishwe hadi kwenye ML. Mathalan, “hazina iliyositirika katika shamba” (Mat. 13:44) ni usemi unaomaanisha “injili na mafundisho yake.” Vinginevyo, tunahoji kuwa mfasiri wa shairi hajafungwa katika matumizi ya tafsiri sisi bali anaweza kutumia mbinu nyingine ilmradi umbo na maudhui wa MC vimehifadhiwa kwa kadiri iwezekanavyo na kuhawilishwa kwenye ML. Aidha tunakumbusha kuwa kizio cha tafsiri katika ushairi wa mshororo.

Ufuatao ni uchanganuzi wa tafsiri ya Zaburi 23 kutoka Kiingereza hadi Kiswahili:

Jedwali 4:1.1 Nafasi ya Matini ya Kishairi katika Kushawishi Mbinu za Tafsiri

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Ushawishi wa Aina ya Matini
A Psalm of David. The Lord is my Shepherd; I shall not want	Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu	Kirai ‘A Psalm of David’ kimedondoshwa yamkini kuepuka utata kuhusu mwandishi wa Zaburi hii ambaye wasomi wa Biblia hawajakubaliana. Vinginevyo, hii ni tafsiri ya kisemnatiki.

He maketh me to lie down in green pastures; he leadeth me beside the still waters	Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza	Hii ni tafsiri ya kimawasiliano.
He restoreth my soul; he leadeth me in the paths of righteousness for his name's sake	Hunihuisha nafsi yangu; na kuniungoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake	Tafsiri ya kimawasiliano imetumikizwa.
Yea, though I walk through the valley of the shadow of death, I will fear no evil: for thou art with me; thy rod and thy staff they comfort me	Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji	Tafsiri ya kimawasiliano imetumikizwa.
Thou prepares a table before me in the presence of mine enemies; thou anointest my head with oil; my cup runneth over	Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu na kikombe changu kinafurika	Halinjeo timilifu imeingizwa mahali pa halinjeo endelevi katika neno “ <i>anointest</i> .” Hii ni tafsiri ya kimawasiliano.
Surely goodness and mercy shall follow me all the days of my life and I will dwell in the house of the Lord for ever	Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele	Tafsiri ya kisemantiki imetumikizwa.

Kutokana na uchanganuzi huu wa Zaburi 23 tumebaini kuwa wafasiri wamefanikiwa kuhawilisha tamathali za semi, picha na sitiari kutoka MC hadi ML. Aidha maumbo ya MC na ML yamesawazishwa. Hii ina maana kwamba wafasiri wamehifadhi idadi ile ile ya, mathalan, sitiari, mishororo, vipande na beti kama ilivyo katika MC. Ama kuhusu nafasi ya matini ya kishairi katika kishawishi mbinu za tafsiri imedhahirika kuwa mbinu za tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki ndizo mbinu mwafaka zaidi za kutumikizwa katika tafsiri za mashairi na zote mbili huweza kutumikizwa katika shairi lile lile. Imebainika kuwa tafsiri za kimawasiliano na kisemantiki huweza kushahibiana au kuonekana ni kitu kile kile hususan pale ambapo matini inatoa ujumbe wa jumla, usiofungamana na utamaduni wa LC, na pale ambapo maudhui ni muhimu sawa na muktadha, mathalan katika mashairi ya kidini kama vile Zaburi 23.

4.2 Uchanganuzi wa Tafsiri ya Mwanzo II

Lengo la sehemu hii ya uchanganuzi wetu ni kubainisha nafasi nduni za simulizi katika kushawishi mbinu za tafsiri. Simulizi kwa mujibu wa Mbatiah (2001) hutoa maelezo, kishairi au kinathari, juu ya matokeo na matendo ya wahusika. Tangu za novella, riwaya na hadithi fupi aghalabu husimulia kwa kutumia msimulizi. Utanzu wa drama hautumii masimulizi kama hayo. Badala yake simulizi hukua kutokana na matendo ya mazungumzo ya wahusika. Mwanzo 20 11:1-9 ni simulizi la kidini kuhusu chimbuko la mataifa na makabila tofauti ya ulimwengu hivyo kubainisha chanzo cha uwili lugha na ulumbi. Hoja muhimu tunayosisitiza ni kuwa katika simulizi sauti, mlio na vihisishi vina umuhimu wa kiwango cha chini vikilinganishwa na hali ilivyo katika ushairi hivyo tafsiri ya simulizi haitakuwa na mwonjo chapwa iwapo mfasiri atashindwa kuzipatia visawe katika LL. Aidha kizio cha maana katika simulizi ni sentensi, lakini yawezekana ikawa hata aya nzima. Hali hii humwezesha mfasiri kunyumbua matini yake ya tafsiri na kuifanya pengine iwe ndefu kupita MC. Hata hivyo tunahoji kuwa ni vema urefu wa simulizi lilotafsiriwa ulingane na ule wa MC na ni vema zaidi iwapo tafsiri itakuwa fupi zaidi, ili kuipatia HL ukweli wa taarifa papo hapo bila kutumia maneno mengi.

Mfasiri hana budi aamue ni maneno yapi ndiyo ya msingi katika MC yake na atafute visawe vyake katika LL. Maneno ya msingi kwa mujibu wa Mwansoko n.w (2015) hugawanyika katika aina mbili ;yale yanayotumika kumjenga na kumbainisha mhusika au kueleza muktadha mahususi wa simulizi na yale yanayombainisha mwandishi mwenyewe na mtazamo wake. Hali kadhalika mfasiri atumie mbinu ya tafsiri itakayozalisha tafsiri nyepesi kwa HL ambayo ama itaruhusu matumizi machache ya tanbihi na sherehe au kuepuka kuvitumia kabisa. Jedwali lifuatalo linawakilisha nafasi ya matini ya kimasimulizi katika kushawishi mbinu za tafsiri.

Jedwali 4.2.1 Nafasi ya Matini ya Kimasimulizi katika Kushawishi Mbinu za Tafsiri

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Ushawishi wa Aina ya Matini
And the whole earth was of one language, and of one speech.	Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja.	Mbinu ya kimawasiliano imetumikizwa: Si kila neno lilotafsiriwa na (mathalan ‘And’) sintaksia ya LL imefuatwa.

And it came to pass, as they journeyed from the east, that they found a plain in the land of Shinar; and they dwelt there.	Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; Wakakaa huko.	Tafsiri ya kimawasiliano imetumika zaidi mbinu ya kisemantiki.
And they said one to another, Go to, Let us make brick, and burn them thoroughly. And they had brick for stone, and slime had they for mortar.	Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa.	Imeegemea zaidi kwenye mbinu ya kimawasiliano.
And they said, Go to, let us build a city and a tower, whose top <i>may reach</i> unto heaven; and let us make us a name, lest we be scattered abroad upon the face of the whole earth.	Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote.	Hii ni tafsiri ya kimawasiliano: Maneno <i>may reach</i> yametafisiriwa kama “kifike” bila italiki yamkini kwa sababu sintaksia ya Kiswahili inaruhusu huo msisitizo bila italiki. Aidha tafsiri ya <i>lest we will be scattered abroad</i> ni “ili tusipate kutawanyika” ambayo inashahibiana na sintaksia ya Kiswahili
And the LORD came down to see the city and the tower, which the children of men builded.	BWANA akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakijenga wanadamu.	Mbinu ya kimawasiliano imetumikizwa
And the Lord said, Behold, the people is one, and they have all one language and this they began to do: and now nothing will be restrained from them; which they have imagined to do.	BWANA akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya	Mbinu ya kimawasiliano imetumikizwa

Go to, let us go down, and there confound their language, that they may not understand one another's language.	Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao.	Tafsiri ya maneno 'Confound' na 'Language' imepoteza maana ya MC: Hii ni tafsiri pungufu. Vinginevyo, imegemea mbinu ya kimawasiliano.
So the LORD scattered them abroad from thence upon the face of all the earth: and they left off to build the city.	Basi BWANA akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kujenga ule mji.	Tafsiri ya kisemantiki: Takriban kila neno limezingatiwa.
Therefore is the name of it called Babel; because the LORD did there confound the language of all the earth: and from thence did the LORD scatter them abroad upon the face of all the earth.	Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo BWANA alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko BWANA akawatawanya waende usoni pa nchi yote.	Tafsiri ya Kisemantiki

Kama uchanganuzi katika Jedwali 4:3.1 unavyoonyesha mbinu mwafaka zaidi inayoweza kutumikizwa katika kutafsiri simulizi na tafsiri ya kimawasiliano. Hutokea mfasiri akaitumikiza mbinu ya tafsiri ya kisemantiki kwa uchache hususan pale ambapo dhamana ya mfasiri ipo kwa mwandishi wa MC badala ya wasomaji wa ML. Aidha tunahoji kuwa tafsiri ya matini ya kisimulizi katu haifai kuwa sisisi kwa kuwa haitoi kwa uangavu maana inayokusudiwa na MC. Tumeonyesha kuwa katika matini ya kisimulizi sehemu yake kubwa huweza kudai aina ya mbinu za tafsiri ya kimawasiliano itumike zaidi ya tafsiri ya kisemantiki.

4.3 Uchanganuzi wa Tafsiri ya Kutoka 20

Kutoka 20:1-17 ni kiwakilishi cha matini elekezi katika utafiti wetu. Kama ilivyo katika matini ya kimjadala nduni muhimu ya matini elekezi na ushawishi (*persuasiveness*). Vandepitte (2008) anahoji kuwa mfasiri hana budi anzingatie nduni hii anapotafuta mbinu mwafaka zaidi ya kutafsiri matini elekezi. Hoja muhimu anayotoa ni kuwa kuwaelekeza wasomaji ni kuwashawishi kufanya jambo kwa namna fulani, ama katika hali fulani au kwa utaratibu fulani.

Matini elekezi huegemea kwa wasomaji kwa njia kadha: matini huibua taswira zinazoteka hisia za wasomaji, mathalan maonyo yanayotangulizwa kwa ishara aina mbali mbali. Wasomaji huingizwa katika uhusiano wa imani: wanazungumziwa kibinafsi, hupongezwa na kuingizwa katika mazingira chanya yenye kuvutia. Matini elekezi pia huibua hamu, mathalan, kwa kumpa msomaji nafasi ya kuchagua bidhaa bora miongoni mwa bidhaa kadha katika matangazo ya kibiashara. Aidha maelekezo hushawishi vitendo: hutoa maelezo kwa nini msomaji afanye jambo kwa namna fulani, hususan, huwaelekeza wasomaji kutenda vitendo kwa utaratibu fulani, kifaa fulani au njia fulani. Tumeeleza kuwa kuna matini elekezi zinazompa msomaji nafasi ya kuchagua atakalo na zile zisizompa nafasi ya kuchagua atakalo. Kutoka 20:1-17 (amri kumi za Mungu) ni kuwakilishi cha matini elekezi zisizompa msomaji nafasi ya kuchagua atakalo. Kutokana na dhima ya matini elekezi tunahoji kuwa tafsiri yake inastahili kuwa nyepesi (mathalan inches-sentimita, gallons-lita) inayozingatia utamaduni na lugha ya HL kwa kadiri inavyowezekana. Muundo wa ujumbe katika ML umwezeshe msomaji kuona utangulizi na seti ya maelezo yenye vitendo anavyohitajika kutenda pamoja na ufafanuzi. Sentensi ziwe sahili na fupi na maagizo yaliyo wazi yatumike kuelekeza mfululizo wa vitendo vinavyohitajika.

Aidha hatua zipangwe kimantiki, mtawalia na ziorodheshwe. Mfasiri anashurutika kuzingatia kuwa ushawishi hufanyika katika mazingira salama na chanya, hivyo utangulizi wa ML sharti ukuze mazingira yasiyo na vitisho na kuwafanya wasomaji kujihisi salama. Pale ambapo maonyo yanahitajika, toni ya ML yafaa kuwa yenye sifa chanya na kuibua matumaini. Kwa kifupi mfasiri wa matini elezi anahitajika kutumia mbinu itakayofanikisha mwingiliano kati ya utamaduni wa HL na ML yenyewe kwa lugha yenye mguso wa kipekee.

Jedwali 4.3.1 Nafasi ya Matini Elekezi katika Kushawishi Mbinu za Tafsiri

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Ushawishi wa aina ya matini
And God spoke all these words; saying, I am the LORD thy God, which have brought thee out of the Land of Egypt, out of the house of bondage.	Mungu akasema maneno haya yote akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wako niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.	Utangulizi huu umetumia mbinu za kisemantiki na kimawasiliano kuibua hisia za usalama, na matumaini.

Thou shalt have no other gods before me.	Usiwe na miungu mingine ila mimi.	Ulinganifu wa kiuamilifu umezingatiwa; tafsiri ya kimawasiliano imetumikizwa.
Thou shalt not make unto thee any graven image, of any likeness of <i>anything</i> that is in heaven above, or that is in the earth beneath, or that is in the water under the earth.	Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia	Tafsiri ya kimawasiliano imetumikizwa.
Thou shalt not bow down thyself to them, no serve them: for I the LORD thy God <i>am</i> a jealous God, visitng the iniquity of the fathers upon the children unto the third and fourth <i>generation</i> of them that hate me;	Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,	Tafsiri imeegemea kwenye maana ya MC, hivyo ni ya kisemantiki.
6. And showing mercy unto thousands of them that love me, and keep my commandments.	Nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.	Taafsiri ya kimawasiliano imebainishwa na neno “nawarehemu” (and showing mercy).
7. Thou shalt not take the name of the LORD thy God in vain; for the LORD will not hold him guiltless that taketh his name in vain.	Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.	Tafsiri ya kimawasiliano imetumikizwa.

8. Remember the Sabbath day, to keep it holy.	Ikumbuke siku ya Sabato uitakase	
9. Six days shalt thou labour, and do all thy work:	Siku ya sita fanya kazi, utende mambo yako yote;	
10. But the seventh day <i>is</i> the Sabbath of the LORD thy God: <i>In it</i> thou shalt not do any work, thou nor thy son, nor thy daughter, thy manservant, nor thy maidservant nor thy cattle, nor thy stranger that <i>is</i> within thy gates:	Lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga wala mgeni aliye ndani ya malango yako.	Utamaduni wa LL umezingatiwa kwa kuingiza maneno kama vile “mtumwa” “mjakazi” na “akaibarikia.” Hivyo kwa kiasi kikubwa tafsiri ya mistari ya 8-11 ni ya kimawasiliano.
11. For in six days the LORD made heaven and earth, the sea and all that in them <i>is</i> , and rested the seventh day: wherefore the LORD blessed the Sabbath day, and hallowed it.	Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na chi, na bahari na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.	
12. Honour thy father and thy mother: that thy days may be long upon the land which the LORD thy God giveth thee.	Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA Mungu wako	
13. Thou shalt not kill.	Usiue.	Tafsiri hii imetumia sentensi fupi na sahili inayozungumza na msomaji papo hapo, hivyo ni ya kimawasiliano

14. Thou shalt not commit adultery.	Usizini.	Maana ya MC haijaitokeza kwa ukamilifu. Vinginevyo, ni tafsiri ya kimawasiliano
15. Thou shalt not steal.	Usiibe.	Tafsiri ya kimawasiliano
16. Thou shalt not bear false witness against thy neighbor.	Usimshuhudie jirani yako uongo.	Tafsiri ya kimawasiliano
17. Thou shalt not covet thy neighbour's house, thou shalt not covet thy neighbors wife, nor his manservant, nor his maidservant, nor his ox, nor his ass, nor anything that is thy neighbour's.	Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alich nacho jirani yako.	Takriban kila neno katika MC limetafsiriwa, hivyo ni tafsiri ya kisemantiki

Uchanganuzi huu wa matini elezi umeangazia ushawishi kama kigezo muhimu kinachoukilia mbinu inayofaa kutumikizwa katika kutafsiri ya matini elezi. Kwa jumla imebainika kwamba tafsiri ya kimawasiliano ndiyo mbinu mwafaka zaidi ya kutafsiri matini elezi. Hoja nyingine muhimu ni kuwa mfasiri anapokusudia kutopotosha ujumbe wa MC, huhitaji kutumikiza tafsiri ya kisemantiki katika baadhi ya sehemu za matini elezi.

4.4 Muhtasari

Sura hii imeangazia nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri. Uchanganuzi wetu umekitwa katika matini za kishairi, masimulizi na matini elezi. Kwa jumla tumebaini kuwa shairi, simulizi ni maagizo haviwezi vikatendewa haki kwa mbinu ya tafsiri sisisi. Maudhui na umbuji wa shairi huweza kuhifadhiwa kwa kiasi kikubwa kwa kutumikiza tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano kwa pamoja katika shairi lile lile. Aidha tafsiri ya kimawasiliano imebainika kuwa bora zaidi katika kutafsiri masimulizi na matini elezi na tafsiri fafanuzi haionekani kupewa nafasi muhimu katika aina zote tatu za matini.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii imelenga kuhitimisa tathmini ya nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri. Kwa mantiki hii tumebaini nduni za matini za kibiblia, (hususan masimulizi matini elekezi na mashairi), usuli wa kihistoria wa matini za kibiblia na mbinu za kuzihakiki. Hali kadhalika tumeangazia matokeo ya utafiti wetu kuhusu nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri na kutoa mapendekezo kutokana na utafiti wetu.

5.1 Muhtasari

Tasnifu yetu imeshughulikia nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za tafsiri. Kazi hii imeshughulikia mada hii kwa kutathmini aina za matini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23. Ili kufanikisha upatikanaji wa mkakati wenye dira, utafiti wetu imechunguza matini hizi katika tafsiri za KJV na SUV. Tumeongozwa na malengo ya utafiti yafuatayo: kuchunguza aina na nduni za matini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23; kuchunguza nafasi ya aina za matini katika kushawishi mbinu za kutafsiri matini za kidini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23; kutambua mbinu za kutafsiri zinazoshawishiwa na aina za matini katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23. Aidha kazi yetu imekitwa katika msingi wa nadharia mbili faafu: Nadharia ya Tafsiri Kielimumitindo na Nadharia ya Tafsiri Kimawasiliano. Nadharia hizi mbili zimeonyesha matokeo yenye natija kwa utafiti wetu.

Katika sura ya kwanza tumetanguliza fasili ya aina za matini hususan katika Biblia na nduni zake. Sura ya pili imechunguza historia ya Biblia na kubaini kuwa uelewa wa historia hii humwezesha mfasiri kuwa katika nafasi bora ya kutekeleza kwa ufanisi shughuli yake ya kutafsiri. Aidha tumehoji kuwa uelewa wa historia ya MC utamwezesha mfasiri kuichambua ipasavyo kwa kuzingatia maneno yake muhimu na mtindo wake wakati wa uhawilishaji wa ujumbe kutoka MC hadi ML. Katika sura ya tatu tumejadili matini chanzi za Biblia, mbinu kadha za uhakiki wa matini hizo na aina za matini. Tumebaini kuwa vipengele hivi ni muhimu katika kumwezesha mfasiri kuteua mbinu mwafaka atakayoitumia kutafsiri matini anayoishughulikia. Sura ya nne imechanganua data ya msingi kwa njia ya jedwali na kuonyesha

mbinu zilizotumikizwa kutafsiri simulizi la Mwanzo II, matini elekezi katika Kutoka 20 na shairi katika Zaburi 23. Kutokana na uchanganuzi huu tumetoa mapendekezo kuhusu mbinu za tafsiri zinazofaa kutumikizwa katika kufasiri aina hizi za matini.

Kwa mintarafu ya mbinu za utafiti, tumetumia maktaba kukusanya data za upili kutoka kwenye vitabu, makala, majarida, intaneti na tasnifu hususan zinazojadili tafsiri za matini za kidini, mitindo yake na ushawishi wa mitindo hii kwa mbinu za tafsiri. Tumekusanya data zinazojadili nadharia ya tafsiri, fasili na aina za matini kisha kuzitumikiza katika kutathmini data za msingi katika Mwanzo II, Kutoka 20 na Zaburi 23.

5.2 Matokeo

Utafiti wetu umeonyesha kwamba kila matini ina upekee wake wa umbo ambalo mfasiri anashurutika kulizingatia ili kufanikisha uhawilishaji wa ujumbe wa MC. Hivyo tumeainisha aina kadha za matini na nduni zinazozitambulisha: matini za kimjadala, matini fasili, dayalojia, maelezo, matini elekezi, mashairi na masimulizi.

Hata hivyo tumebaini kuwa matini nyingi huwa ni mahuluti (hybrid). Kwa mantiki hii shairi linaweza kuwa na simulizi, matini ya kimjadala inaweza kuwa na nduni za matini fasili na matini elekezi huweza kuwa na nduni za matini ya kimaelezo. Tunahoji kuwa ulinganifu katika tafsiri si suala la maneno na sentensi tu bali pia kuna kiwango cha umbo la matini kwa kuwa aina tofauti za matini zina uamilifu tofauti wa kimawasiliano.

Uchanganuzi wa Zaburi 23 umebaini kuwa tafsiri ya kinathari haifai kutumikizwa katika kutafsiri mashairi kwa kuwa husababisha kupotea kwa umbuji na maana ya MC. Aidha mtafsiri wa shairi anahitajika kutambua kuwa matumizi ya lugha ya kitamathali na polisemia ni nduni muhimu ya MC ambayo haina budi ihawilishwe kwenye ML. Ama kuhusu nafasi ya matini ya kishairi katika kushawishi mbinu za tafsiri, utafiti wetu unaelekea kuonyesha kuwa mbinu za tafsiri ya kimawasiliano na tafsiri ya kisemantiki ndizo mbinu mwafaka zaidi za kutumikizwa katika tafsiri za mashairi na zote mbili huweza kutumikizwa katika shairi lile lile. Hali kadhalika imedhihirika kuwa mbinu ya tafsiri sisisi katu haifai kutumikizwa katika kutafsiri mashairi.

Tafakuri yetu kuhusu nafasi ya matini ya kimasimulizi katika kushawishi mbinu za tafsiri ni kuwa aina hii ya matini humpa mfasiri nafasi ya kunyumbua matini yake ilimradi simulizi la MC na lile la ML liwe na ulinganifu wa maana. Hivyo utafiti wetu umeonyesha kuwa mbinu za tafsiri ya kimawasiliano ndiyo mbinu mwafaka zaidi inayoweza kutumikizwa katika kutafsiri simulizi. Tumeonyesha kuwa tafsiri ya kisemantiki hutumikizwa kwa uchache katika tafsiri ya simulizi hususan pale ambapo mfasiri ameegemea kwa MC badala ya wasomaji wa ML.

Imebainika kuwa nduni muhimu ambayo mfasiri wa matini elekezi anashurutika kuzingatia ni ushawishi. Tumehoji kuwa kuwaelekeza wasomaji ni kuwashawishi wafanye jambo kwa namna fulani, ama katika hali fulani au kwa utaratibu fulani. Hivyo tafsiri ya matini elekezi sharti iegemea kwa HL kwa kutumia mbinu itakayoshawishi vitendo, hisia, na imani fulani. Kwa mantiki hii imebainika kuwa tafsiri ya kimawasiliano ndiyo mbinu mwafaka zaidi ya kutafsiri matini elekezi. Pale ambapo mfasiri anapokusudia kutopotosha ujumbe wa MC, atahitaji kutumikiza tafsiri ya kisemantiki kwa umakinifu.

Kwa jumla, utafiti wetu, umeelekea kuonyesha kuwa aina ya matini ni kipengele muhimu kinachoshawishi mbinu za tafsiri. Hivyo tunahoji kuwa uelewa wa uanishaji wa matini za tafsiri una natija kwa wafasiri kwa kuwa huwezesha kubaini mbinu mwafaka ya kutafsiri matini ya aina fulani.

5.3 Mapendekezo

Imedokezwa kwamba utafiti wetu umekitwa katika nafasi ya aina za matini na nduni zake katika kushawishi mbinu za tafsiri. Kwa kuzingatia upeo na mipaka ya kazi yetu masuala kama vile rejesta, ulinganifu wa maana, utamaduni na historia ya LC yamepembeza ijapokuwa yana uhusiano muhimu na utafiti wetu.

Kwa mantiki hii tunapendekeza kuwa utafitiwa kina zaidi wa mada hii ufanywe utakaohusisha vipengele hivi muhimu. Aidha kwa kuwa Biblia ni matini yenye ukwasi wa aina za matini tunapendekeza kuwa aina za matini ambazo hazikushughulikiwa katika utafiti wetu zifanyiwe utafiti. Hivyo kwa kuwa hili ni eneo ambalo halijafanyiwa utafiti wa kutosha tunapendekeza lipewe ilhamu kwa kutafiti kuhusu aina nyingine za matini kama vile matini za kimjadala, matini

fasili na matini za kimaelezo. Tumemaliza kwa kupendekeza kuwa utafiti zaidi ukifanywa utachangia sana kupambanua uelewa wa ushawishi wa aina za matini katika kushawishi mbinu za tafisiri na kuzalisha marejeleo faafu yanayoweza kukuza eneo hili la utafiti.

MAREJELEO

- Aichele, G. (2001). *The Control of Biblical Meaning: Canon as Semiotic Mechanism*. Harrisburg: Trinity Press International.
- Alter, R. (2010) The Glories and the Glitches of King James Bible: Ecclesiastes as a Test Case. In Hamlin, Hannibal and Jones, Norman. *The King James Bible after 400 Years: Literary, Linguistics and Cultural Influences*. Cambridge: CUP. Vol 45. pg. 45-58.
- Arege, T. (2013). *Tunu ya Ushairi*. Nairobi Oxford Univeristy Press (East Africa) Ltd.
- Baker, M. (2006). *Translation and Conflict: A Narrative Account*. London. Routledge.
- Bhatia, V. (2002). *Applied Genre Analysis: A Multi-perspective Model* Iberica 4: pp3-19. Hong Kong: Association Europea de Lenguas Para Fines Especificos (AELFE).
- Boase-Beier, J. (2012). *Stylistic and Translation*. In Malmkjaer and Windle (ed). *The Oxford Handbook of Translation Studies*. Retrieved on 3rd April, 2013 from www.oxfordhandbooks.com.
- Bronn, D. (2013). *One Bible, Many Versions: Are All Translations Created Equal?* Downers Grove, IL: IVP Academic.
- Cairns, E. (1996). *Christianity Through the Centuries. A History of the Church*. Michigan: Zondervan.
- Delabastita, D. (1993). *There is a Double Tongue: An Investigation into the Translation of Shakespeare's World play with Special reference to Hamlet*. Amsterdam: Rodopi.
- Edwards, D. (1997). *Christianity: The First Two Thousand Years*. London: Cassell.
- Edwards, J. (2009). *The Hebrew Gospel and the Development of the Synoptic Tradition*. Cambridge: Wm. B Eerdmans Publishing Company.
- Elohists Texts. Retrieved on 11th May 2017 from barrybandstra.com/tables/pt1/pt1-tb3-hm.
- Four Types of Narrative. Retrieved from <https://artisinitiative.org/online-course-2> on 6th June 2017.

- Ganz, M. (2008). What is Public Narrative. Retrieved from Chutzpahportfolio.yolasit.com/resources/Whats/public Narrative08.pdf on 30th May 2017.
- Gonza'lez, J. (2010). *The Story of Christianity, Volume I: The Early Church to the Reformation*. New York: Harper Collins Publishers.
- Goswell, G. (2011) One More Translation of the Holy Scriptures: Robert Alter and the King James Bible (1611). *The Reformed Theological Review*. Vol. 70/3 pg. 206-219.
- Hatim, B. na Mason, I. (1990) *Discourse and the Translator*. Essex: Longman Group UK. Limited.
- Hunter, E. (2013). Language, Empire and the World: Karl Roell and the History of the Swahili Bible in East Africa. In the *Journal of Imperial and Commonwealth History*. Vol. 41, No. 4, 600-616.
- Jeffrey D.L. (2012). Translation and Transcendence: The Fragile Future of Spiritual Interpretation in *Modern Theology* 28/4 pp. 688-706. Waco: Backwell Publishing Ltd.
- Keene, M. (2002). *The Bible*. Oxford: Lion Publishing PLC.
- Kerber, D. (2016). The Canon in the Vulgate, Translation of the Bible. In the *Bible Translator*. Vol. 67(2). 168-183.
- Malangwa, P. (2014). *Challenges of Translating Cultural Expressions in Teaching Kiswahili to Foreigners*. In *Kiswahili* Vol. 77:104-117. Dar es Salaam: TATAKI.
- Malmkjaer, K. (2004). *The Linguistic Encyclopaedia* (2nd ed.) London: Routledge.
- Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi :Fotoform Ltd.
- Mojola, A.O. (2000). *The Swahili Bible in East Africa (1844-1996)*. *The Bible in Africa: Transactions, Trajectories, and Trends*. West G., Dube M. (ed.) Boston: Brill Academic Publishers. Inc.

- Muruga, N. (2012). *Translation Challenges of Swahili Plays: A Case Study of Maua Kwenye Jua La Asubuhi* by K. Wamberia (2004) and *Kinjeketile* by Ebrahim Hussein (1969). University of Nairobi (Unpublished Thesis).
- Musau, O. (2011). Collaborative Web-Based Computer-Assisted Bible Translation Software: A Prototype. University of Nairobi (Unpublished Thesis).
- Mwansoko H., Mekacha R., Masoko D., Mtesigwa P. (2015). *Kitangulizi cha Tafsiiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Obeng, E. (1997). The Use of Biblical Critical Methods in Rooting the Scriptures in Africa. In Kinoti and Wliggo (ed). *The Bible in African Christianity*. PP. 8-14. Nairobi: Hetion Publishers.
- Ondara, R. (2010). Ufaafu wa Maana katika Tafsiiri ya Nyimbo Dini. *Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta* (Haijachapishwa).
- Otwere, S. (2011) Usonde katika Tafsiiri. *Tathmini ya Mafundisho ya Biblia katika Shule ya Sabato kwa Watu Wazima. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi* (Haijachapishwa).
- Priestly source. Retrieved on 11th May 2017 from https://www.revolvy.com/topic/priestly_source & Item-type= topic.
- Q source. Retrieved on 15th May 2017 from <https://en.m.wikipedia.org>
- Reiss, K. (2004). Type, Kind and Individuality of Text: Decision Making in Translation. In Venuti L. *The Translation Studies Reader*. New York: Routledge.
- Religious Texts*. Retrieved on March 22, 2017 from https://en.m.wikipedia.org/wiki/Religious_Texts
- Ruzaita, J. (2006). Text Typology in Translation. A Case Study of Menu Translations. Retrieved from Article (EN). Pdf on 25th May 2017.
- Ryken, L. (2002) .*The Word of God in English: Criteria for Excellence in Bible Translations*. Wheaton: Crossway.
- Timeline of the New Testament Books. Retrieved on 19th April 2017 from www.bible-history.com/new-testament.

Trosberg, A. (2002). Discourse Analysis of Part of Translater Training. In Sch'a'ffner C. The Role of Discourse Analysis of Translation & in Translater Training (ed.) Clevedon: Multilingual Matters Ltd.

Vandepitte, S. (2008). Translating Instructive Texts. In Hermes- Journal of Language and Communication Studies 40 (5).

Vilhanova, V. (2006). Biblical Translators of Early Missionaries in East and Central Africa: Translations into Swahili. In Asian and African Studies. Vol. 15 No. 1, 80-89.

Wales, K. (2001). *A Dicitonary of Stylistics* .Harlow: Pearson Educatin Limited.

When was the Old Testament Written? Retrieved on 18th April 2017 from www.biblestudy.org/beginner/when.was-old-testament-written.html

Yahwist Source. Retrieved on 11th May 2017 from: <https://www.britamica.com/topic/yawhist-source>.